Nipashe
Jumamosi Mei 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581673
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




UKURASA 11

**Mwenyekiti** UVCCM abanwa kauli uchochezi

UKURASA 4

**Maofisa** h/shauri mbaroni madai ya kuwatesa wananchi

UKURASA 4

**Watano** wafariki dunia kuangukiwa na kifusi mgodini

UKURASA 5

# Bunge lataka riba mifuko ya hifadhi uchelewaji mafao

UKURASA 2



"Kuna watumishi wanaostaafu kwa sasa wanasotea mafao kuanzia miezi sita hadi mwaka." – Spika Tulia.

## Makonda aagiza Nyumba iliyouzwa mil. 3/- irejeshwe



UKURASA 3

## ACT yasema bajeti haitoshi kumaliza tatizo la maji nchini

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAPANIA KUTANGAZA UBINGWA DODOMA UK.24

**MAONI,** UK.6



Waziri Kivuli wa Maji wa Chama cha ACT-Wazalendo, Yasinta Awiti, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Maji katika maeneo sita. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Bunge lataka riba mifuko kuchelewesha mafao

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameshauri serikali kuandaa mpango wa kubadili sheria ili kuweka riba kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii itakayochelewesha mafao kwa wastaafu.

Dk. Tulia aliyasema hayo jana baada ya majibu ya Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliyekuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema wapo wastaafu waliokuwa kwenye Mfuko wa Akiba wa Wafanyakazi (NPF) na baada ya kuanzishwa mifuko ya PSSSF na NSSF mafao yao yalihamishiwa huko, lakini wana madai ya muda mrefu hadi leo hawajalipwa na kuhoji kauli ya serikali.

Akijibu swali hilo, Katambi aliomba mbunge ampe taarifa ya watumishi hao kwa kuwa taarifa zinaonyesha madeni yaliyorithiwa na NSSF na PSSSF mwaka 2018 zaidi ya asilimia 78 wamelipwa na wengine malipo yao yanaendelea kufanyiwa uhakiki.

"Hakuna sehemu kubwa ya malalamiko ya watu ambao walionyesha taarifa zao ni sahihi na wote walishalipwa," alisema.

Kutokana na majibu hayo, Spika Tulia alisema kuna watumishi wanaostaafu kwa sasa wanasotea mafao kuanzia miezi sita hadi mwaka.

"Kuna wanaostaafu hivi sasa wanasubiri miezi mitatu, sita, mwaka. Kwa sababu inajulikana anastaafu lini, mtu miezi sita hajapata mshahara ili maisha yake aliyokuwa nayo hapo nyuma yasishuke, anatakiwa kufanyaje wabunge wanachoka kupokea ujumbe kwa nini hamjajipanga muda wote mtu akistaafu aanze kulipwa fedha zake?" alihoji.

Akifafanua hoja ya Spika, Katambi alisema serikali ilishaboresha na taarifa za wastaafu zinaandaliwa miezi sita kabla ya kustaafu na ndani ya siku 60 mstaafu analipwa mafao yake.

Hata hivyo, Spika Tulia alisema: "Ushauri wa jumla kama ambavyo waajiri wakichelewesha sheria inataka walipe riba, kwa upande wa mifuko wanapomcheleweshea mtu fedha nao wawekewe riba ili wawe wanawahisha.

"Kwa hiyo tunawatarajia kwenye mabadiliko ya sheria ili wakibanwa nao hawatachelewesha fedha za wananchi," alisema.

KIKOKOTOO

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Ngara (CCM), Ndaisaba Ruhoro, alihoji serikali ina mpango gani wa kuirekebisha kanuni ya kikokotoo ili kuongeza kiwango cha mafao ya mkupuo kwa wastaafu.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mafao ikijumuisha malipo ya mkupuo kwa wastaafu.

"Sheria inaitaka mifuko kufanya tathmini ya kupima uhimilivu kila baada ya miaka mitatu na kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ikiwamo maboresho ya mafao ya wanachama na kanuni mpya ilianza kutumika Julai 2022,"alisema.

Alisema ni muhimu kuzingatia ushauri wa wataalamu kuhusu uendeshaji, usimamizi na uendelevu wa mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kuwa unazingatia utaalamu wa sayansi ya watakwimu - bima (actuarial science).

Pia alisema uamuzi wa kubadilisha Kanuni ya Kikokotoo cha Mafao ya Wastaafu ni lazima utokane na tathmini ya kina ya kisayansi ya watakwimu bima kama ilivyoelezwa na Makamu wa Rais, wakati wa Sherehe za Mei Mosi, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Malinyi (CCM), Zeno Mgungusi, alihoji kama serikali haioni haja ya kurejesha fao la kujitoa kwa watumishi na kupatiwa michango yao mara tu wanapoacha kazi bila kusubiri umri wa miaka 55 au 60.

Naibu Waziri Katambi, alisema mfumo wa kinga ya jamii unalenga katika kuhakikisha wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii wanapata sifa ya kulipwa pensheni badala ya michango yao.

"Hata hivyo, inapotokea mwanachama kuondoka kazini kabla ya umri wa kustaafu, serikali imetayarisha Kanuni za Mafao za Mwaka 2023 ambazo zinamwezesha wanachama kupata mafao ya mkupuo maalum kulingana na sifa alizo nazo kwa wakati huo," alisema.

Alisema lengo kuu la serikali ni kuwakinga wananchi wake dhidi ya majanga kama umaskini uliokithiri, uzee, ugonjwa na kukosa kipato.

Katambi rai kwa wananchi kuwa na utamaduni wa kuendeleza uchangiaji wao katika mifuko ya hifadhi ya jamii wanapobadilisha waajiri, ili kutopoteza haki yao ya kupata pensheni pindi wanapostaafu.

# ACT yasema bajeti haitoshi kumaliza tatizo la maji nchini

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema katika uchambuzi wake, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2024/25, haitoshi kumaliza tatizo la maji nchini.

Kutokana na hali hiyo, chama hicho kimetoa hoja sita kuhusu nini kifanyike katika kumaliza tatizo hilo.

Kimesema katika uchambuzi wake umeonyesha, miradi mingi bado haijakamilika na ile iliyokamilika baadhi haitoi maji, huku kasi ya wananchi kuvuta maji ikionesha ni ndogo kutokana na gharama kubwa za kuunganishwa na huduma hiyo.

Kutokana na mwenendo huo, Waziri Kivuli wa Maji wa chama hicho, Yasinta Awati, jana wakati akichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2024/25, alisema chama kinapendekeza serikali itenge Sh. trilioni 10 kwa miaka mitano ili kumaliza kero za maji.

Katika hoja yao ya kwanza inayohusu kasi ndogo ya usambazaji na upatikanaji duni wa maji mijini na vijijini, Awati alisema mahitaji ya maji kwa umma yanaongezeka kwa asilimia saba kila mwaka, lakini uzalishaji wake umeongezeka kwa asilimia 2.6 kwa mwaka 2024/25.

"Sababu kubwa ya uzalishaji kuwa chini ni uwezo mdogo wa Wizara ya Maji kusimamia miradi mbalimbali ya maji na ufinyu wa bajeti. Hii ni kutokana na miradi mingi ya maji kutokamilika kabisa au kuzalisha kiwango kidogo cha maji. Kwa mwaka wa fedha wa 2024/25, uzalishaji wa maji nchini ni asilimia 58 tu ya uhitaji wa maji wa wananchi," alisema.

Alisema hilo limesababisha tatizo la upatikanaji wa maji au tatizo la mgawo na kupelekea wananchi kutumia muda mwingi na gharama kubwa .

Pia alisema hali ya upatikanaji wa huduma za maji safi na salama vijijini ni asilimia 79.6 tu na hizo zinatajwa kwa maana miradi iliyofika siyo upatikanaji wa huduma ya maji.

Alisema taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS 2023) inaonyesha miradi ya maji iliyowekezwa vijijini takribani asilimia 38 haifanyi kazi kwa ufanisi au imekoma kabisa kutoa huduma na zaidi ya vijiji 497 havijafikiwa na mradi wowote wa maji.

Kutokana na changamoto hiyo, Yasinta alisema chama chao kinaitaka serikali itoe ruzuku kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ili kuziwezesha kupanua usambazaji na kuboresha miundombinu katika maeneo yao.

Kadhalika, alisema wizara isimamie uwajibikaji wa mamlaka hizo na kuwachukulia hatua watendaji na wasimamizi wanaozembea katika kuhakikisha upatinaji wa uhakika wa maji kwa wananchi.

Katika hoja yao ya pili inayohusu mwendelezo wa uzembe na ubadhirifu wa fedha za miradi ya maji, Awiti alisema kila mwaka wa ukaguzi wa matumizi ya fedha zinazoidhinishwa na serikali kwa ajili ya miradi mbalimbali, wizara hiyo imekuwa ikikutwa na hoja zenye thamani ya mabilioni ya shilingi zilizotafunwa.

Pia alisema katika mwaka ulioishia Juni 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ameonyesha maeneo ya uzembe yaliyosababishia mamlaka mbalimbali hasara.

Alisema kutokana na kasoro zilizojitokeza katika matumizi mabaya ya fedha za umma, ACT Wazalendo imemtaka Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ajitathmini kama anafaa kuendelea kuiongoza wizara hiyo muhimu kwa maslahi mapana ya wananchi.

"ACT Wazalendo inaitaka serikali kuwawajibisha wakandarasi, watendaji na watumishi wote waliohusika na uzembe huu," alisema.

Katika hoja yao ya tatu inayohusu gharama kubwa, kubambikiwa ankara na ucheleweshaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi, Yasinta alisema chama chao kinaunga mkono mfumo wa mita za malipo ya kabla na kuitaka serikali kuzigharamia na kuwafungia wananchi ambao wanalipia huduma za maji.

Kadhalika, wameitaka serikali itangaze bei elekezi na nafuu ya kuunganishwa na huduma ya maji mijini na vijijini, ili iwe rahisi wananchi kuvuta maji majumbani.

"Hoja yetu ya nne ni kuchelewa kukamilika miradi ya maji, ACT Wazalendo tunataka wizara itengewe Sh. trilioni mbili kila mwaka yaani Sh. trilioni 10 kwa miaka mitano kumaliza kabisa tatizo la maji nchini," alisema.

Yasinta alisetaja hoja ya tano ni hasara kubwa ya upotevu wa maji Sh. bilioni 324.39, huku chama hicho kikiitaka serikali kufanya ukaguzi na ukarabati wa miundombinu kama vile, mita, mabomba, matanki, kuzuia upotevu wa maji na pia, kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa wananchi unafika kwa wakati.

Pia, alisema mamlaka zichukue hatua za haraka kufanya ukaguzi na ukarabati katika maeneo ambayo yana uvujaji na upotevu wa maji.

Katika hoja yao ya sita inayohusu mifumo mibovu ya maji taka katika miji, alisema utafiti unaonyesha ili kupata ufanisi katika usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa taka kunahitaji bajeti ya kutosha, ambapo iliyotengwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya usimamizi wa mifumo ya taka ni finyu.

"Tunaitaka serikali iongeze jitihada ya kibajeti na kiusimamizi katika uboreshaji wa miundombinu katika miji ili kuwezesha mifumo ya maji taka ya moja kwa moja kwa kujenga mitaro mikubwa itakayopita mijini," alisema.

Yasinta alisema pia, alisema hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa wabebaji wa maji taka watakapobainika kuyatirirsha mitaani.

## HABARI KITAIFA

# Makonda aagiza nyumba iliyouzwa mil. 3/- irejeshwe

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, ameagiza kurejeshwa kwa nyumba ya Kalisti Nassoro, yenye thamani ya zaidi Sh. milioni 50 iliyouzwa na madalali kinyume cha utaratibu kwa Shilingi milioni tatu.

Kadhalika, ameagiza madalali wote wakiwamo wa mahakama wanapokwenda kukamata mali za wananchi kutoa taarifa kwenye ofisi ya wilaya husika.

Akisikiliza kero za wananchi katika operesheni maalum iliyoanza Mei 8, mwaka huu hadi jana, jijini Arusha, Makonda alisema kulikuwa na kesi ya mtu aliyeuziwa nyumba yake kwa mkopo wa Kijenge Saccos.

"Nilikutana na mwenyekiti wa ile Saccos, ofisa mikopo na watendaji, hawajawahi kutoa kibali cha kuuzwa kwa ile nyumba," alisema.

Makonda alisema mwanasheria amejiridhisha na wamemjulisha, hawakubaliani kuuzwa kwa nyumba hiyo na mhusika alipatiwa kibali cha kukusanya madeni sio kwenda kuiuza.

"Nimeagiza akamatwe, ashitakiwe na bahati nzuri, Taasisi ya Kuzua na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ilifanya uchunguzi ikabaini, hana mamlaka ya kuuza nyumba ile, nyumba inarejeshwa kwa mmiliki.

"Mambo haya huwezi kuyaona kama upo ndani unakunywa wine (mvinyo) hujui shida za wananchi, lazima tukubaliane ndiyo maana sheria imempa nafasi kiongozi kusikiliza kero za wananchi," alisema.

Nyumba ya Nassoro iliuzwa mwezi Oktoba, mwaka 2016, akiwa katikati ya kurejesha mkopo bila kushirikishwa katika tukio hilo na kutolewa vitu vyake nje na mifugo.

"Ninataka niwajulisha madalali wote wa mahakama, lazima tuwasajili na kuwatambua, na hakuna kufanya jambo lolote katika eneo la Arusha bila kujulisha Mkuu wa Wilaya katika eneo lake husika ili tubaini matapeli.

"Tunapowahudumia wananchi wasikasirike, wakati tunapewa maelekezo ya kusikiliza kero za wananchi hatukuambiwa usikilize kero gani na kero fulani usisikilize," alisema.

Makonda alisema mtaalamu wa sheria yupo na wote kwa pamoja wakiulizwa wanajua Mkuu wa Mkoa kwa cheo chake ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mwenendo wa Nidhamu wa Mahakama za Mwanzo katika mkoa wake.

"Ana nafasi ya kusikiliza malalamiko ya wananchi alafu Jaji Mfawidhi katika ngazi yangu ya mkoa ni mjumbe kwenye kikao changu au ni katibu. Ninadhani sheria ipo wazi, kwa maana kama una malalamiko umeenda mahakamani ukaona hakimu amehukumu akiwa amelewa una haki ya kuja kwa Mkuu wa mkoa," alifafanua.

Makonda alisema Sheria Na. 4 ya Uendeshaji wa Mahakama ya Mwaka 2011 imeunda vyombo mbalimbali vya kusimamia kwa mujibu wa sheria hiyo, Mkuu wa Mkoa ndiye mwenye wajibu wa Mwenyekiti wa Maadili wa Mkoa.

"Kama kuna kiongozi aliwadhulumu akisikia tangazo la Mkuu wa Mkoa Arusha, wananchi wote waliodhulumiwa waje, unafikiri huyo kiongozi anafanyaje.

"Si anaanza kupiga simu kwa watu, 'Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, hili jambo analolifanya Makonda lipo kwa mujibu wa taratibu' hapo anataka kumpiga presha waziri wangu kumuonyesha ninachokifanya siyo sahihi.

Ama anapiga simu kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Biteko, 'huyu kijana tumuangalie' kumbe aliyepiga simu ni mwizi mla rushwa na kupora mali za watu."

"Atajidai kupiga simu kwa viongozi wangu utadhani ana jambo la maana, wewe kama una jambo la maana mtafute Makonda, mshauri aboreshe nini, wananchi wapate haki zaidi," alisema.

"Kupiga simu kwa viongozi wangu wakubwa na kupeleka video kwamba, nitatengeneza mgogoro kati ya mahakama na serikali, kasomeni sheria ya mwaka 2011, imenipa mamlaka na nafasi ya kusikiliza na yale nitakayoyabaini nitamwambia Jaji Mfawidhi," alisisitiza.

Makonda alisema moja ya ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ni kuhakikisha wanaongeza msukumo wa upatikanaji wa haki ili kuongeza faraja kwa wananchi.

Alisema kwa mujibu wa ilani, katiba ya nchi na sheria ya utawala, yupo sahihi kuwasikiliza wananchi na kutatua kero, huku akieleza kama hawataki afanye hivyo, wang'oe vifungu.

**AONYA MATAPELI**

Alisema yupo mwananchi ambaye ametapeliwa kiwanja chake alichouziwa Sh. milioni 26 ambacho kiliuzwa kwa mtu mwingine na amekuwa akihangaika kupatiwa haki yake kwa muda mrefu.

"Huyu mtu ameingia katika anga zangu, nilisema kwenye suala la haki ni mara kumi kurudi nyumbani nikalee watoto wangu watatu kuliko kukaa kwenye kiti cha watu wanalia na kunyanyasika huku nikichekelea kuitwa Mkuu wa Mkoa, hii haina faida wanashindwa kupata haki kwa vile hawatoi rushwa hii sio sawa."

Makonda alisema aliwasiliana na mwanasheria ambaye alimweleza kuwa, mhusika amekiuka kwa kujipatia mali wa njia ya udanganyifu na kuagiza akamatwe.

"Jana amekuja, tayari amekabidhi eneo la watu. Kama upo katika mkoa huu, kuna tapeli anajiandaa kufanya utapeli namwomba ahame nikimkamata kwenye kumi na nane zangu, sitajali wewe ni nani ilimradi sheria, taratibu na kanuni zinazompatia kila mtu haki zake," alionya.

Alisema kama viongozi wanatakiwa kusimamia haki za wananchi na watatangaza vituo vya sheria ili kila mwananchi asiingie kwenye mkataba ama manunuzi yoyote kabla ya kupatiwa msaada wa kisheria.

"Kuna hili tukio limeniuma sana wamepewa eneo na kaka yao wakajenga nyumba mtu na mume wake. Mume amefariki dunia, jamaa ameenda kuvunja nyumba akachukua kiwanja chake, fikiri angewapata wanasheria wangemtengenezea utaratibu leo hii tungejua pakuanzia," alisema.



Vigezo na Masharti Kuzingatiwa

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

HABARI KITAIFA



Fundi wa Shirika la Ugavi la Umeme nchini (TANESCO), akikarabati nyaya za umeme kwenye nguzo eneo la Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwenyekiti UVCCM abanwa kauli uchochezi

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Kagera, wamemtaka Mwenyekiti wa jumuiya hiyo mkoa, Faris Buruhan, kuomba radhi au kujiuzulu nafasi yake kwa matamshi yake ya hivi karibuni kutaka kuwapoteza watu wanaotukana viongozi mitandaoni.

Buruhani alitoa kauli hiyo hivi karibuni akiwa kwenye ziara katika mji mdogo wa Rulenge wilayani ya Ngara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani hapa, kijana ambaye ni kada wa chama hicho, Mohamed Ismail, alisema kauli hiyo imewashangaza watu wengi na isipochukuliwa hatua, watu wabaya wanaweza kuitumia kuichafua serikali ambayo haikumtuma kusema maneno hayo.

Ismail alisema vijana wa mkoa huo wanasikitishwa na kauli iliyotolewa na mwenyekiti wa UVCCM wa Mkoa huo na kwamba wanalaani kauli hiyo inayoleta taswira mbaya na kuwaweka kwenye wakati mgumu vijana wa chama hicho.

Alisema kauli ya mwenyekiti huyo imekiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 77 inayompa kila mtu haki ya kuishi na kwamba ingawa wanapinga watu wanaotukana mitandaoni, si busara kusema atawapoteza.

Kada mwingine wa CCM, Innocent John, alisema hata Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, alikemea kauli hiyo mara tu alipoitoa lakini wanamshangaaa hajajitokeza na kuomba radhi hadharani ingawa muda umepita.

"Dk. Nchimbi akiwa mikoa ya kusini alikemea kauli hiyo akisema ni ya kijinga lakini mwenyewe amekaa kimya. Kwa hiyo sisi tulitarajia baada ya kauli ya Dk. Nchimbi ambaye ndiye mtendaji mkuu wa chama, Buruhan angejitokeza na kuombaa radhi lakini amekaa kimya tu hali inayoonyesha dharau sasa hii itatuletea shida sisi vijana, " alisema John

"Tunaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa 2025. Sasa anapozungumza Mwenyekiti wa UVCCM Kagera inaonekana hilo jambo linatuwakilisha sisi wote. Kwa hiyo lazima ajitokeze aombe radhi na akishindwa ajiuzulu,.

"Kwa maslahi mapana ya nchi yetu tunamwomba ajiuzulu kama ameshindwa kuomba radhi kwasababu limeleta taharuki na itatusumbua sisi kwenye chama," alisema.

> **"Kwa maslahi mapana ya nchi yetu tunamwomba ajiuzulu kama ameshindwa kuomba radhi kwasababu limeleta taharuki na itatusumbua sisi kwenye chama," alisema.**

Kijana mwingine wa UVCCM, Ibrahm Rweyongeza, alisema moja ya kanuni za maadili ya chama hicho inasema kazi ya kiongozi wa chama ni kulinda chama, kukijenga na kukilinda, kuwa na maadili na kutotenda maovu na kuwa na maadili na kutimiza wajibu wake.

"Ibara ya tano ya Kanuni za UVCCM inasema kazi ya umoja huo ni kulinda na kujenga ujamaa, ujamaa tunaujua unasema watu wote ni sawa hakuna mwenye mamlaka ya kumpoteza mtu yeyote kwa hiyo tunaona mwenzetu amekwenda kinyume na maadili ya chama chetu," alisema Rweyongeza.

"Sisi vijana tunaomba Buruhan ajitokeze hadharani aombe radhi laakini kama atashindwa kufanya hivyo aachie ngazi kwasababu si kwamba anatuharibia sisi wanaCCM mkoa wa Kagera tu anaharibia vijana wa nchi nzima. Kazi ya UVCCM ni kupika viongozi na viongozi wenye maadili mema siyo wa aina hii," alisema.

Alisema Dk. Nchimbi aliwahi kuwa Mwenyekiti wa UVCCM kwa muda mrefu na alifanya kazi kwa uadilifu hali ambayo imewavutia viongozi kumpa nafasi mbalimbali za uongozi na sasa ni Katibu Mkuu wa CCM, hivyo wanataka kuona vijana wanafuata mfano wa Dk. Nchimbi.

## Mbaroni madai kuwatesa walipa ushuru

**Na Vitus Audax**

MAOFISA watano wa kitengo cha ukusanyaji mapato katika Halmashauri ya Msalala, Kahama mkoani Shinyanga, wametiwa mbaroni kwa tuhuma za kuwatesa na kuwaadhibu wananchi wanaodaiwa kukwepa kulipa ushuru wa mazao.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, amethibitisha kukamatwa kwa maofisa hao ambao hawakutajwa kwa majina kwa njia ya simu akiwa safarini, baada ya kudaiwa kuhusika katika kipande cha video kilichosambaa mitandaoni kikionyesha watumishi wakiwatesa wananchi mbele ya halmashauri hiyo.

Mhita alikiri jana kupokea kipande hicho cha video na kuwa baada ya kukipata serikali ilichukua hatua kupitia jeshi la polisi wilayani hapa ambao walifika kwa wakati na kuwakamata watumishi hao kwa taratibu zaidi za kisheria.

"Wahusika wako watano ambao ni watumishi wa ukusanyaji wa kodi na Mei 7, mwaka huu, walipelekwa polisi wakapata dhamana na mpaka sasa suala hilo liko mikononi mwa polisi. Kuhusu suala la utumishi wao tumewapumzisha tukipisha uchunguzi kwani kitendo hicho si maelekezo ya serikali," alisema Mhita.

Aidha, alisema katika kipande hicho cha video, ilibainika kuwa watumishi hao waliwapa adhabu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaviringisha katika mchanga la kuwarusha kichurachura na kutaja hatua hiyo kuwa si jukumu lao kujichukulia sheria mkononi.

"Ni kweli tuko katika ukusanyaji wa mapato na tunayahitaji zaidi lakini si kwa namna hiyo waliyoitumia watumishi hao kwani ziko njia mbalimbali zikiwamo kuwaelimisha na wananchi wanajitoa na wanahitaji elimu zaidi lakini kile si jukumu lao kama maofisa," alisisitiza.

Aliwataka watumishi wote kufanya kazi kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa sheria katika hatua za ukusanyaji mapato na wala si kujichukulia sheria mkononi.

Juzi bungeni, Mbunge wa Msalala, Idd Kassim, aliweka mezani hoja hiyo ili Bunge liahirishe shughuli zake na kuanza kuijadili kwa kile alichokieleza kuwa wakulima jimboni kwake wanaviziwa wakitoka shambani na kudaiwa ushuru kinyume cha utaratibu.

Hoja hiyo pia iliibuliwa na Mbunge wa Sengerema, Hamisi Tabasamu, aliyeilitaka Bunge kujadili juu ya hatua hizo alizozitaja kuwaumiza wananchi na wakulima jimboni kwake.

Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, aliiagiza serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kufuatilia suala hilo katika halmashauri husika na kulitolewa maelekezo.

Pia alisema kwa mujibu wa sheria, ushuru wa mazao unatozwa pale mhusika anapokwenda kuuza mazao husika wala si shambani, hivyo kutoa wiki moja serikali kutoa maelekezo juu ya utaratibu huo.

# Mgodi Alcaeda waua watu watano, kujeruhi wanne

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

WATU watano wamefariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa wilayani Ulanga, mkoani hapa baada ya kuangukiwa na ngema na kufukiwa na kifusi wakati wakichimba madini katika Mgodi wa Alcaeda.

Taarifa zilizopatikana wilayani humo na kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Kamishna Mwandamizi wa Polisi (SACP), Alex Mkama, zilisema tukio hilo lilitokea Mei 8, mwaka huu, katika mgodi huo, Kata ya Nawenge, wilayani Ulanga.

Kamanda Mkama aliwataja wachimbaji waliofariki dunia kuwa ni, Ishiwa Kadege (30), mkazi wa Tabora, Ismail Bashiri (35), mkazi wa Arusha, Stephen Mpiondi (34), mkazi wa Epanko Ulanga na Shabani Andrea, mkazi wa Masasi, Mtwara na miili yao imehifadhiwa Hospitali ya Ulanga.

Alisema uchunguzi kuhusu tukio hilo unaendelea ikiwamo kujua kama mgodi huyo upo kihalali au la.

"Kuna baadhi ya wachimbaji huwa wanakwenda hadi chini kabisa na hivi sasa mvua inaendelea kunyesha, lakini pia ardhi haijajishika vizuri, kwa hiyo mtikisiko wowote ukitokea, lolote linaweza kutokea. Kwa hiyo kwa tukio hili, udongo ulijimega na kuwafunika waliokuwa chini na kusababisha wakose hewa na kufariki dunia," alisema Kamanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ruby International Limited katika mgodi wa Epanko wanaomiliki pia, Mgodi wa Alcaeda, Betold Matambala, alisema ajali hiyo ilisababishwa na kumegeka kwa mwamba, huku akikanusha kuwa ajali hiyo kusababishwa na mvua inayoendelea.

"Ajali ilitokea saa kumi jioni. Shughuli za uchimbaji hutekelezwa kwa kutumia vilipuzi, hivyo kulitokea mtikisiko na kusababisha jiwe kumegeka na kuwafunika wachimbaji," alifafanua Matambala.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Alex Mkama, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Morogoro jana. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Bashungwa aitaka TEMESA kuongeza ubora

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ameutaka Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), kubadilisha mtazamo wao katika utoaji huduma ili waweze kujiendesha kibiashara kama sekta binafsi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za usafiri wa vivuko nchini.

Bashungwa alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati alipoikutanisha TEMESA na Kampuni ya M/S Azam Marine, kujadili namna ya kuendelea kushirikiana kwa pamoja kuboresha utoaji wa huduma za usafiri wa vivuko katika eneo la Magogoni- Kigamboni.

Kikao hicho kiliwakutanisha Katibu Mkuu wa Ujenzi, Balozi Mhandisi Aisha Amour, timu ya wataalam kutoka TEMESA na uongozi wa Azam Marine, ukiongozwa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Azam Marine, Abubakar Aziz.

"TEMESA nyie ni watoa huduma, hivyo lazima mbadili mitazamo yenu na kujiendesha kama sekta binafsi sambamba na kuweka mifumo madhubuti itayosaidia utoaji wa huduma zenu kuwa bora," alisema waziri huyo.

Kaimu Mkurugenzi Uendeshaji na Ujenzi wa Vivuko kutoka TEMESA, Mhandisi Sylvester Simfukwe, alisema TEMESA ililazimika kutafuta njia mbadala ya kuhakikisha huduma inaendelea katika eneo la Magogoni-Kigamboni mara baada ya Kivuko cha MV. Kazi kupelekwa kufanyiwa ukarabati mkubwa.

Alisema waliingia makubaliano na Kampuni ya Azam Marine ya kushirikiana kutoa huduma ya usafiri wa vivuko kulingana na mahitaji.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Azam Marine, Abubakar Aziz alisema Azam kwa sasa wanakodisha Sea tax mbili kwa TEMESA katika kituo cha Magogoni -Kigamboni, ambavyo vinatoa huduma masaa manane kwa siku na kusafirisha abiria 3,000 kwa saa na abiria 24,000 ndani ya siku moja.



## Watano akiwamo mhadhiri wa chuo mbaroni tuhuma za ubakaji watoto

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro linawashikilia watu watano akiwamo mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Jordan, mjini hapa Morogoro kwa tuhuma za kuhusika na matukio ya ubakaji na ulawiti kwa watoto katika maeneo mbalimbali ya mji.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Morogoro Kamishna mwandamizi wa Polisi, SACP, Alex Mkama, alisema miongoni mwa waliokamatwa ni mtumishi wa chuo kikuu cha Jordan, Stanley Mbena (39), mkazi wa Kola A Manispaa ya Morogoro anayetuhumiwa kumlawiti mtoto wake mwenye umri wa miaka tisa. Alisema tukio hilo lilitokea Mei 3 mwaka huu.

Alimtaja mtuhumiwa mwingine kuwa ni Alex Doglas mwenye umri wa miaka 34 mkazi wa Kigurunyembe, Manispaa ya Morogoro, anayedaiwa kumbaka mtoto wake wa miaka 12 ambaye ni mwanafunzi wa shule ya msingi Kigurunyembe, Mei 2, mwaka huu.

Alisema watuhumiwa wengine watatu wanahusishwa na matukio ya ubakaji na wote walikamatwa ikiwa ni jitahada za jeshi hilo katika kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Uchunguzi unaendelea na ukikamilika watuhumiwa hawa wote watafikishwa mahakamani," alisema SACP Mkama.

Aliwaasa wazazi kuwa karibu na watoto wao ili waweze kugundua viashiria wanapofanyiwa vitendo vya ukatili na kupewa vitisho.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya watu wa karibu na familia ya mhadhiri wa Jordan walisema awali mama wa mtoto anayedaiwa kulawitiwa alikuwa akimuogesha mwanawe na kugundua anatoka uchafu sehemu za haja kubwa na alipombana alidai kufanyiwa vitendo hivyo na wanafunzi wenzake shuleni.

Walisema aliamua kumpeleka mtoto wake shuleni ili walimu wamhoji na kubaini watoto hao, lakini walimu walipombana alimtaja baba yake mzazi kuhusika na kwamba tukio la mwisho alimpatia Sh. 30,000 akimuonya asiseme.

Inadaiwa pia baba na mama wa mtoto huyo walitengana kutokana na changamoto za kimahusiano na mama kuondoka na watoto wao wote watatu, wakiwamo wadogo zake anayedaiwa kufanyiwa ukatili, lakini baadaye baba aliwachukua wote kwenda kuishi nao.

Taarifa zaidi zikadai kuwa mzazi huyo wa kiume baada ya kugundua tukio hilo limefikishwa shuleni, aliwaambia baadhi ya walimu walipuuze kwasababu mzazi mwenzie alikuwa na tatizo la ugonjwa wa akili.

Ilidaiwa mzazi huyo wa kike hakuwa akijua kama mumewe alihusika na tukio hilo na alikwenda shuleni ili walimu wasaidie kuwabaini watoto wanaodaiwa kuhusika na vitendo hivyo, kabla ya baadaye shuleni kugundua mhusika na mumewe.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utulivu, busara wahitajika dirisha la usajili likikaribia

**WAKATI** msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa 2023/2024 ukitarajiwa kumalizika ifikapo Mei 28, mwaka huu, tayari klabu mbalimbali zimeshaanza mchakato wa kusajili wachezaji wapya kwa ajili ya kuwatumia kwenye msimu mpya.

Usajili huo wa wachezaji utahusisha pia Ligi ya 'Championship' ambayo tayari imemalizika kwa KenGold ya Jijini Mbeya kutwaa ubingwa na kupanda daraja rasmi sambamba na Pamba Jiji FC ya Mwanza iliyoshika nafasi ya pili.

First League au Ligi Daraja la Pili kama ilivyozoeleka pamoja na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania pia hutakiwa kufanya usajili wa wachezaji wake katika dirisha hilo ambalo hutambuliwa rasmi na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Huu ni wakati muhimu kwa klabu kufanya mipango ya kujiimarisha wakati kwa upande wa wachezaji kila mmoja huitaji kupata timu inatayompatia dau nono la usajili lakini pia mshahara mnono wa kila mwezi.

Kipindi cha usajili ni kipindi kinachohitaji utulivu kwa timu kwa sababu ndio kitakachotoa taswira ya kikosi chake kuelekea msimu mpya kama kitafikia malengo au kitakuwa kimecheza pata potea.

Usajili wa wachezaji unaweza kuita pia ni kitendo cha bahati na simu au 'kubeti' kwa sababu baadhi ya klabu husajili wachezaji waliowika katika klabu zao na wanapofika kwao mambo huwa tofauti na hadi kufikia hatua kuambiana wamesajili 'bomu' kutokana na kushuhudia kiwango cha chini cha nyota husika.

Na kwa upande wa wachezaji unaweza kukuta anakubali kuingia mkataba na timu iliyompa kiwango kikubwa cha pesa lakini akiwa hana uhakika na kupata namba hali ambayo hupelekea kushusha kiwango chake na kupoteza jina lake lililokuwa limeshakaa 'midomoni' mwa mashabiki wake wa soka.

Kitu muhimu ni kila upande kuhakikisha inakuwa makini na inaweka mbele busara katika kukamilisha mchakato huu muhimu ambao ndio hutoa hatima ya mafanikio ya msimu mpya wa mashindano.

Timu zinatakiwa kufanya usajili kwa kuzingatia mashindano mbalimbali yaliyoko mbele yao na si kwa kukomoana baada ya kufahamu mpinzani wake ana dhamira gani.

Usajili wa kukomoana mara kadhaa umeonekana ama kuigharimu klabu kwa kutumia fedha ambazo wangewekeza katika jambo lingine au kumgharimu mchezaji aliyehusika kwa kushindwa kupata kila alichokitarajia.

Huku klabu ikipoteza fedha kwa kumhudumia mchezaji ambaye amesajiliwa nje ya mipango ya benchi la ufundi, kwa mchezaji yeye huenda akajipotezea au akajiondoa kwenye ubora wake kutokana na changamoto atakazokutana nazo kwenye timu mpya.

Mchezaji mwenye malengo hawezi kukubali kusajiliwa na timu kwa kuangalia upande mmoja wa maslahi, atalazimika kuongozwa na busara katika maamuzi yake ambayo hatayajutia katika siku za usoni kwa sababu atakuwa ameweka mbele maendeleo ya kipaji chake.

Lakini bila kusahau kusajili wachezaji wakigeni wenye ubora na viwango vya juu vitakavyowasaidia nyota wazalendo kukutana na changamoto mpya, klabu zinatakiwa kutofukuza hovyo makocha kwa kufuata 'kelele' za mashabiki ambao asilimia kubwa hawana weledi wa kubaini uwezo halisi wa walimu hao.

Klabu zenye timu za wanawake pia zinatakiwa ziweke kipaumbele usajili wa kuboresha vikosi vya timu za wanawake ambazo pia kwa sasa ligi yake imekuwa na ushindani kutokana na wachezaji kuonyesha uwezo mkubwa kwa kutotabiri mshindi wa mechi tofauti na ilivyoanza ambapo timu zilikuwa zinafungana idadi kubwa ya mabao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Timu ziongezwe Ligi ya Wanawake

**LIGI** Kuu Tanzania Bara ina timu 16, 'Championship' nayo ina idadi hiyo hiyo ya timu.

Ligi Daraja la Pili 'First league' ina timu 16, zinazogawanywa makundi manne, baadaye kila kundi zinatoka timu mbili na kuunda timu nane, ambazo nazo zinakuwa katika makundi mawili.

Hapo utagundua kuwa ligi zote hizo zina timu zaidi ya 15. Ni Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ndiyo ina timu 10 tu.

Kwa maana hiyo timu zinacheza mechi chache sana na akina dada wanalazimika kukaa muda mrefu bila kucheza soka.

Ukiwa na ligi ya timu kumi, ina maana timu zinacheza mechi 18 tu, tisa kila mzunguko kati ya mizunguko miwili.

Tuliona baada ya kumalizika mzunguko wa kwanza, kulikuwa na mapumziko marefu mno, kiasi kwamba kuna baadhi ya mashabiki wakaanza kujiuliza kama ligi hiyo imemalizika, au imesimamishwa.

Ni hivi karibuni tu mzunguko wa pili umeanza, lakini zimebaki raundi tatu tu ili ligi hiyo ifikie mwisho.

Binafsi naona idadi ya timu 10 kwenye Ligi Kuu ya soka Wanawake ni ndogo sana ikilinganishwa na ukubwa wa ligi yenyewe.

Mimi nadhani labda Ligi Daraja la Pili ndiyo ingekuwa na timu 10, lakini Ligi Kuu ya Wanawake, angalau ingekuwa na kuanzia timu 12 hivi, mpaka 14.

Nina sababu nyingi za kutetea hili. Kwanza kabisa ikumbukwe kuwa ligi ya wanawake kwa sasa imeshaanza kukubalika miongoni kwa mashabiki wa soka nchini tofauti na zamani.

Hivi sasa tunaona uwanjani mashabiki wakijazana kwenda kuangalia timu za wanawake zikicheza.

Hata mashabiki wa Simba na Yanga, wamekuwa wakiziunga mkono timu zao za wanawake, Simba Queens na Yanga Princess ingawa si kwa kiwango kile kile kama wanachofanya kwenye timu za wanaume.

Tunaona baadhi ya mashabiki wa Simba wale wale wanaoonekana wakati timu ya wanaume ikicheza wakiwa na ngoma zao, wakiisapoti timu ya wanawake, Simba Queens kila inapocheza hapa Dar es Salaam, kiasi cha kuwafanya akinadada hao kujisikia fahari na kila mechi inapokwisha wanakwenda kuwashukuru.

Hivi sasa mashabiki kwenye vibanda umiza wanalipa viingilio na wanakuwa wengi wakati timu Simba Queens au Yanga Princess zinacheza mechi zao, na hata zinapocheza 'dabi' upinzani, au ushabiki unakuwa ni ule ule kama wa timu za wanaume.

Kinachotakiwa hapa sasa ni mamlaka za soka, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kutafuta wadhamini tu kwa ajili ya kuziwezesha timu hizo kujiendesha na wachezaji kupata malipo mazuri.

TFF ina uwezo huo, kwani ina kitengo chake cha biashara, na yapo makampuni yanayotengeneza bidhaa zinazoendana na wanawake kama taulo za kike, nguo, vipodozi, sabuni, na hata bidhaa za watoto, ambayo yakikaribishwa vizuri na kuelezwa faida zake, yanaweza kuwekeza.

Uwepo wa timu nyingi kwenye Ligi Kuu, utasababisha wachezaji kupata wakati mwingi wa kucheza soka na kuwa imara kwani timu bingwa anakwenda kuiwakilisha nchi kwenye mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), na baadaye kama ikiwa bingwa, inauwakilisha ukanda kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo wachezaji wanahitaji mechi nyingi kwa ajili ya kuwa fiti zaidi.

Kama msimu wa 2020/21 ambako hakukuwa na mwamko wowote wa soka la wanawake kulikuwa na timu 12, kwa nini msimu huu ambao wengi wameonekana kulikubali soka la wanawake kuna timu 10 tu?.

Nadhani TFF waliangalie hili, wakati umefika wa kuongeza timu, msimu ujao angalau ziwe 12, na unaofuata ziwe 14 kwa ajili ya kuleta msisimko na ushindani.

# Walia upungufu wa wataalamu dawa usingizi

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha Wanataaluma Watoa Dawa za Usingizi na Ganzi Tanzania (SATA), kimesema licha ya serikali kuweka miundombinu ya kutosha katika kada yao, lakini inakabiliwa na upungufu wa wataalamu wa dawa za usingizi ambapo kwa sasa wapo 85 kati ya 1,200 wanaotakiwa kuwapo.

Rais wa chama hicho, Dk. Edwin Lugazia, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa mwaka wa nane wa chama hicho.

"Serikali imeweka miundombinu ya kutosha ya usingizi salama ikiwamo mashine za kutosha pamoja na vitendea kazi pamoja na dawa za kutosha, lakini bado tunakabiliwa na chagamoto ya kutokuwa na watoa huduma wenye weledi wa kutosha," alisema Dk. Edwin.

Hata hivyo, alisema katika kukabilina na chagamoto hiyo, wamekuwa wakijengeana uwezo katika aina tofauti za upasuaji, ikiwa ni pamoja na namna ya kutoa usingizi salama, pamoja na kuwahudumia wagonjwa mahututi ambao wanahitaji dawa za usingizi.

"Kwa sasa vituo vingi vimeongezwa, tunahitaji kukimbizana kufundisha watoa huduma ambao wataweza kutoa huduma hizi kila mahali," alisema.

Dk. Lugazia alisema kupitia mkutano huo ambao unafanyika kwa siku mbili na kujumuisha washiriki 250, watajadiliana na kupata mafunzo ya vitendo kwa nadharia na kubadilisha mawazo.

"Mkutano huu umekuwa ukifanyika kila mwaka kwa wanataaluma kwa lengo la kujadiliana na kubadilisha uzoefu sambamba na mafunzo tofauti pamoja na kujengeana uwezo katika ngazi ya chini mpaka ya juu hadi ya kimataifa," alisema Dk. Edwin.

Pia alisema kupitia mkutano huo watajadiliana changamoto wanazokumbana nazo pamoja na zile zinazokabili taifa katika huduma za kutoa dawa za usingizi na wagonjwa mahututi na kutafuta mbinu mbadala za kukabiliana nazo.

Katibu Mkuu wa SATA, Dk. John Kweyamba, alisema madaktari bingwa ambao wamekuwa wakiingia katika chama hicho wamekuwa wakipata fursa mbalimbali zilizolenga kuwajengea uwezo zaidi.

"Wataalamu hawa wanapojiunga na chama chetu wamekuwa wakipata fursa ya kwenda kujiendeleza katika nchi mbalimbali ambazo wana uhusiano nazo kama chama na kuiwezesha nchi kupata wataalamu wabobezi zaidi," alisema Dk. Kweyamba.

Alisema licha ya kuwapo kwa changamoto, chama kimekuwa kikizifanyia kazi na kupata suluhisho ikishirikiana na serikali.

"Tunakiri kuwa changamoto zipo, lakini kwa sasa zimepungua kutokana na madaktari bingwa nchini kuongezeka. Tumekuwa tukiwajengea uwezo katika mikoa hasa wauguzi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi," alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Kweyamba alitoa wito kwa wataalam kuzidi kungana pamoja ili kujenga taifa lenye wataalam bora na kutengeneza afya bora za wananchi.

# Ummy awa mbogo kadi kliniki kuuzwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya Ummy Mwalimu, amesema anakerwa na tabia iliyozuka katika hospitali na vituo vya afya kuuza kadi za kliniki kwa wajawazito na watoto chini ya miaka mitano kinyume cha Sera ya Afya.

Kutokana na hali hiyo amepiga marufuku tabia ya watumishi katika kada hiyo muhimu kuuza kadi hizo.

Ummy alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye hafla ya ugawaji wa vitabu vya kufuatilia maendeleo ya mama mjamzito na watoto chini ya miaka mitano, iliyofanyika kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

"Kuna jambo ambalo linanikera sana. Hivi sasa kadi za kliniki kwa ajili ya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano hazipatikani. Wanasema hazipo lakini kadi zinauzwa na sera inasema kadi ni bure. Nasisitiza Katibu Mkuu Wizara ya Afya sitaki kusikia mjamzito anauziwa kadi ya kliniki.

"Mjipange leo hapa tunagawa kadi milioni 1.2 lakini kwa mwaka makadirio ya mahitaji ya kadi ni milioni 1.4. kati ya bidhaa ambazo sitaki kusikia haipatikani ni kadi hizi za kliniki kama nilivyoelekeza kwenye upatikanaji wa damu hata kama bajeti itatoka kidogo mhakikishe kadi zinakuwapo za kutosha. Moja ya vitu vya kipaumbele ni kadi za wajawazito na watoto chini ya miaka mitano," alisisitiza.

Pia alisema waganga wakuu lazima wafuatailie usambazji wa kadi pamoja na makisio yao ya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano kwa mwaka.

Akizungumzia kuhusu hali ya wajawazito kuhudhuria kliniki, alisema kwa hivi sasa asilimia 80 ya wanaenda kliniki angalau mara nne katika kipindi chao cha ujauzito.

"Lakini bado hatufanyi vizuri kwa kuwa mahudhurio ya kwanza ni asilimia 41 tu ndiyo wanahudhuria chini ya wiki 12 au miezi mitatu tangu kupata ujauzito. Twendeni tukahamasishe kinamama kwenda kliniki mapema.

"Ukiwahi kuna changamoto ya kuzaa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi unazipunguza, hivyo kama mama mwezi wa kwanza hujaona wageni (hedhi), wa pili hujaona wageni, basi nenda kliniki utafanyiwa vipimo na kama mjamzito utaanza kliniki mapema," alisema.

Kadhalika, alisema upatikanaji wa vitabu vya kliniki kwa ajili ya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano utatumika kuwapima utendaji wa Katibu Mkuu Wizara ya Afya pamoja na yule wa Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

"Naelekeza mjipange vizuri kuhakikisha vitabu hivi vinapatikana mapema kwenye maeneo yote. Hilo ndilo tutampima Katibu Mkuu Afya na TAMISEMI. Hii kero tunaimudu kuitatua, hatupaswi kuona upungufu wa vitabu vya kliniki nchini," alisema.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa kituo cha mabasi ya mwendokasi, eneo la Posta Mpya, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yaandaa mfumo mmoja wa kodi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema serikali inaendelea na mchakato wa kuandaa mfumo mmoja wa ukusanyaji wa kodi kwa wafanyabiashara ili kuondoa kero ya taasisi mbalimbali za serikali kukusanya kodi.

Alisema hayo jana jijini hapa kwenye mkutano wa majadiliano kati ya sekta za umma na sekta binafsi uliokuwa na lengo la kujadiliana namna ya kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara nchini.

Dk. Kijaji alisema kero hiyo imekuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu na wafanyabiashara na wadau mbalimbali kuwa ilikuwa ikichangia kuua biashara na kufukuza wajasiriamali na wawekezaji.

"Kilio hiki tumeshakisikia na serikali tunaendelea na majadiliano ya kuanzisha mfumo mmoja wa kukusanya mapato. Yatakusanywa kwenye kapu moja kisha kila taasisi itapata mgawo wake, hivyo kupunguza usumbufu," alisema Dk. Kijaji.

Pia alisema Tanzania na Marekani zimeanzisha chemba moja ya wafanyabiashara nchini Marekani kurahisisha ushirikiano wa biashara na kupunguza mlolongo wa usafirishaji wa bidhaa mbalimbali.

Aliwataka Watanzania kuwa waaminifu kwenye biashara ili kuepuka kuharibu masoko ya kimataifa akidai kuwa fursa hiyo ya soko la marekani ni muhimu kulindwa pamoja na masoko mengine ya kimataifa.

Waziri Kijaji alisema wizara inaendelea na mazungumzo na Shirika la Ndege la Uturuki kwa ajili ya kuanza usafirishaji wa maparachichi yanayozalishwa nchini kwenda uturuki ambako kuna soko kubwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, alisema wizara hiyo imekuwa ikishirikiana na vyombo mbalimbali kufanya oparesheni za kukamata bidhaa bandia zinazoingizwa nchini ili kulinda viwanda vya ndani na afya za wananchi.

Alisema hivi karibuni walifanya ukaguzi kwenye mikoa mbalimbali nchini na kuwakamata baadhi ya wafanyabiashara wakiuza simu feki, hivyo kuwachukulia hatua za kisheria ikiwamo kutaifisha bidhaa hizo na kuwasweka ndani.

Aliagiza taasisi zinazohusika na usimamizi wa ubora wa bidhaa nchini kuendelea kuchukua hatua kwa wale wanaokiuka ili kukuza viwanda vya ndani na kulinda usalama wa wananchi.

"Hatuwezi kuacha watu wanaingiza bidhaa feki nchini. Bidhaa hizo ni hatari kwa uchumi wetu na kwa maisha ya wananchi. Kwa hiyo niwahakikishie kwamba tutaendelea kuchukua hatua maana usalama wa Watanzania uko mikononi mwetu," alisema Abdallah.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Mbeya, Erick Sichinga, alisema utitiri wa kodi umekuwa ukisababisha kutoelewana kati ya wafanyabiashara na taasisi za serikali.

Alisema baadhi ya taasisi zinazokusanya kodi na tozo zimekuwa zikifanya kazi bila kuwashirikisha watu wa sekta binafsi ili na wao watoe maoni yao hali ambayo inaendelea kusababisha migogoro.

Alisema moja kati ya taasisi ambazo zimekuwa zikiwakwamisha wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Taasisi ya Afya na Usalama mahali pa kazi (OSHA) ambazo zimekuwa zikiwatoza tozo kubwa.



Mkurugenzi wa shirika la Akili Platform, Roghat Robert (katikati) akishiriki kupanda miti na Mwalimu wa Shule ya Msingi Kitete, Manispaa ya Tabora, Marcyana Chidemi (kushoto) na baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wakati wa zoezi la kupanda miche ya miti shuleni hapo, juzi. Zaidi ya miche 300 ya miti ya matunda ilipandwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge lapitisha bajeti Wizara ya Maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limepitisha Bajeti ya Wizara ya Maji ya Sh. bilioni 627.78 kwa mwaka 2024/25, huku likiagiza Kamati ya Bajeti kufanya majadiliano na serikali kuhusu hoja tatu zilizoibuliwa na wabunge ikiwamo kutoridhishwa na kupunguzwa kwa bajeti hiyo.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alilazimika kutoa maelekezo hayo baada ya Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Halima Mdee, kuomba mjadala wa wizara hiyo uahirishwe hadi Jumatatu ili kuruhusu Wizara ya Fedha kukaa na Kamati ya Bajeti kuangalia maeneo ambayo yanahitaji kuongezewa fedha.

Katika maelezo yake, Mdee alisema michango iliyotolewa na wabunge inazungumza namna ambavyo wizara imepewa bajeti pungufu ya bajeti ya Sh. bilioni 137.

"Bunge tukipitisha bajeti hii itaonyesha bajeti ni pungufu hatutaweza kumwambia Waziri wa Fedha aongeze, hivyo tunaomba liahirishwe hadi Jumatatu ili kamati ya bajeti ikae na wizara ya fedha tuambiwe kiasi hicho cha fedha kinapatikana wapi ili kujazia fedha zilizoombwa,"alisema Mdee.

Hata hivyo, Spika Tulia alisema pamoja na kupitishwa makadirio hayo, kuna nafasi ya kufanyika marekebisho kupitia Kamati hiyo kabla ya kusomwa kwa bajeti ya serikali.

Akiahirisha kikao cha Bunge, Spika Tulia alisema hoja zingine za wabunge ni kupendekeza kuongezwa kwa sh. 50 kwa lita ya mafuta, kamati hiyo itakwenda kuangalia kama tatizo ni fedha kutokwenda kwa wakati licha wizara kutengwa.

Spika alisema kabla ya kupendekeza ongezeko hilo, mijadala imeashiria kwamba fedha haziendi wizara ya maji licha ya kutengwa na zinazotoka kwenye mfuko ni vyema kanuni ya ugawaji unafanyikaje. "Kamati yetu ikatazama hilo, kwamba fedha iongezeke kwenye mafuta ama isiongezeke, kama tatizo ni kanuni ya ugawaji kamati ilitizame vizuri, kama ni fedha kutokwenda haitakuwa na uhusiano na kuongezeka kwa sh. 50 ili fedha ziende kwa mujibu wa taarifa aliyotoa Waziri wa Maji kuwa zipo fedha nyingi ambazo zipo wizarani kwa ajili ya kufanya miradi mbalimbali.

"Kwa hiyo tutaipelekea kamati yetu ifanye hivyo, na hoja nyingine ambayo imezungumzwa hapa kuhusu RUWASA ambayo ndio inaingia kwenye kanuni ya ugawaji kwa sababu hadi sasa inapewa licha ya kutopewa kwa utaratibu ambao unaweza kuleta tija," alisema.

"Suala hilo litapelekwa kwa kamati ikalitazame kwa sababu kuenda fedha alizoeleza waziri kwamba zinatoka Benki ya Dunia na wadau wengine inawezekana inakuja kwa sura inabidi bajeti ipungue,"alisisitiza.

Alibainisha kuwa hatua hiyo itawezesha bunge kufanya maamuzi kwa kutumia kanuni ya 124 na kuwatoa wasiwasi wabunge kuwa kamati itafanyia kazi.

Awali, katika mjadala wa bajeti hiyo, Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, alishauri uongezwaji wa bajeti ya maji hadi kufikia Sh. trilioni 1.5 kwa kuwa sekta yam aji inagusa watu wengi.

"Bunge lisimame kidete kutetea bajeti ya Wizara ya Maji ambayo imepungua kutoa Sh.Bilioni 756.2 kwa mwaka 2023/24 hadi Sh.Bilioni 627.7 kwa mwaka 2024/25, hii haikubaliki na ni kinyume cha nia ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani kwa maana ya kumaliza changamoto ya maji nchini," alisema.

Mbunge wa Mwibara (CCM), Charles Kajege alisema bajeti ikiongezwa itasaidia Wizara kutekeleza majukumu yake ya kusambazia wananchi maji kwa ufanisi.

Naye Mbunge wa Maswa Mashariki (CCM), Stanlaus Nyongo alisema kitendo cha Rais kupeleka maji vijijini ni hatua muhimu ya mapambano dhidi ya magonjwa ya kuambukiza.

Nyongo alisema ukipeleka Dola moja kwenye maji, unakuwa umeokoa Dola nne kwenye kumtibu mtu ambaye anapata huduma ya maji.

Mbunge wa Donge (CCM), Soud Mohamed Juma, alisema watanzania wanaona namna wizara inavyofanya kazi ya kuhakikisha huduma za maji zinaboreshwa kwa wananchi huku akishauri bajeti kuongezwa na sera ya maji ya mwaka 2002 ifanyiwe maboresho kwa maana ina miaka 20 sasa ili kuendana na mwelekeo mpya wa huduma za usambazaji maji.

Kwa upande wake, Mbunge wa Bukene (CCM), Selemani Zedi aliungana na wabunge wengine ambao hawaridhishwi na bajeti hiyo ya maji kupungua na hivyo kuishauri serikali kuongeza bajeti ya maji kwa kuwa ni sekta muhimu kwa wananchi.

"Kuna tatizo lingine pia,pamoja na bajeti ya maji kupungua hata hiyo iliyopangwa maeneo mengi haiendi kikamilifu kama ilivyopangwa,kwa mfano katika halmashauri yangu ya wilaya ya Nzega huu mwaka unaoisha mwezi ujao tulitarajia kupata bilioni 10 za maji lakini mpaka sasa umebaki mwezi mmoja tumepata bilioni tano tu, ushauri wangu kwa serikali maji ni muhimu mno na fedha zote zinazopangwa kwa ajili ya maji zinapaswa kwenda kwa asilimia 100,"alisema Zedi.

# Serikali yasikia kilio cha makandarasi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesikia kilio cha wabunge kuhusu makandarasi wanaotekeleza miradi ya maji nchini kutolipwa fedha zao kwa wakati kwa kutoa Sh. bilioni 68 ili kulipa madeni yao.

Akijibu hoja za wabunge katika mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji, Waziri Jumaa Aweso alisema kutokana na michango ya wabunge, Wizara ya Fedha imetoa hakikisho la kuwalipa makandarasi hao ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi.

"Niwaombe wakandarasi mmeona jinsi wabunge walivyowapigania, mmesikia kilio cha wabunge namna wanavyowatetea niwaombe sana fedha hizi tumezipata, ) nendeni mkafanye kazi, tutaendelea kuwa marafiki kwa wanaofanyakazi na wale wasiofanyakazi tunaendelea kushughulika nao ili kufikia azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani," alisema.

Alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, kusimamia ulipwaji wa makandarasi huku akiwataka wahandisi wa maji wa mikoa na wilaya kutoibua visingizio.

Kadhalika, Aweso alisisitiza moja ya kipimo cha wakurugenzi wa mamlaka za maji ni kuhakikisha katika maeneo hayo hakuna upotevu wa maji na huduma kwa wateja zinaimarika. Naye, Naibu Waziri Mhandisi Kundo Mathew, alisema Wizara ya Maji imejipanga katika miradi ya visima 900 vitakavyochimbwa majimboni itakamilika ndani ya miezi sita ili watanzania wapate majisafi na salama.

Awali, Mbunge wa Bahi (CCM), Kenneth Nollo, alisema ili miradi ya maji ikamilike kwa wakati na kumnufaisha mwananchi, serikali inapaswa kuwalipa wakandarasi wazawa kwa wakati. "Kumekuwa na changamoto katika kuwalipa wakandarasi wazawa kwa wakati, hali inayochochea miradi mingi kushindwa kukamilika katika muda uliopangwa,"alisema.

Kadhalika, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Bulaya alilalamika vyombo vya ulinzi na taasisi za serikali kuwa na madeni makubwa wanayotakiwa kulipa kwa kutumia huduma ya maji.

Alisema taasisi za serikali zinadaiwa Sh.Bilioni 26 na kuhoji kwanini wasisitishiwe huduma kama wananchi wanavyokatiwa kwa kutolipa ankra za maji.

"Mheshimiwa Spika kwa mfano Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanadaiwa Sh. bilioni 12, Magereza Sh. bilioni sita, Polisi Sh. bilioni 5.3, serikali za mitaa Sh. bilioni 1.5, hospitali za nikoa Sh. milioni 635, Ikulu ndogo Sh. milioni 102 na Mifugo Sh. milioni 44,"alisema.



## Kampeni kupinga njaa kuzinduliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la World Vision Tanzania linatarajia kuzindua kampeni ya Enough kwa ajili ya kupinga njaa kwa watoto katika maeneo mbalimbali nchini ili kuwasaidia watoto kukua vizuri.

Mkurugenzi Mtendaji World Vision, James Anditi, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye mkutano na wadau wa. masuala ya lishe.

Alisema shirika hilo limedhamiria kupambana na tatizo la lishe kwa watoto shuleni na nyumbani.

"Tumekutana na wadau kutoka serikalini kuangalia jinsi ambavyo tunaweza kuendeleza ile kampeni ambayo inaitwa Enough inayowapa nafasi wananchi kuangalia jinsi gani wanaweza kukomesha mambo ya njaa na utapiamlo kwa watoto kuanzia umri wa mwaka moja hadi nane,"alisema.

Alisema takwimu zinaonyesha kwamba baadhi ya mikoa kama Njombe, Iringa na Rukwa bado ina kiwango kikubwa cha utapiamlo licha ya kuwa na uzalishaji mkubwa wa mazao na kwamba hatua zisipochukulia, watoto hawatakua vizuri.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Watoto kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Sebastian Kitiku, alisema ili mtoto akue vizuri, anahitaji kupata lishe bora.

"Tunawashukuru sana World Vision Tanzania kwa kuja na hii kampeni ya kuhamasisha masuala ya lishe kwa kipindi cha mwaka 2024 mpaka mwaka 2026, tunaamini kampeni hii tukiisimamia vizuri itatuletea matunda ambayo tunatarajia na tutajivunia Watanzania wote,"alisema.

Alibainisha kuwa asilimia 90 ya ukuaji wa ubongo wa binadamu unakua kwa kipindi cha mwaka 0 mpaka miaka 8 na moja ya vitu ambavyo vinasisitizwa ni lishe bora.

"Lakini kuna mikoa mingine inakwenda mpaka asilimia 56 maana yake nusu ya watoto walio katika Mkoa huo wanakabiliwa na changamoto za utapiamlo hiyo siyo ishara nzuri,' alisema.

Mtaalam wa Afya na Lishe kutoka World Vision Tanzania Kanda ya Kati, Salome Mtango, alisema lishe si tu kula na kushiba bali ni muhimu kujua makundi sita ya vyakula wanavyokula.

# FCT yasajili mashauri 443 migogoro ya biashara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Ushindani wa Biashara (FCT) limesajili mashauri 443 yanayotokana na migogoro ya kibiashara na kati ya hayo, 429 yamesikilizwa na kutolewa uamuzi katika kipindi cha Mwaka 2007 hadi Machi, mwaka huu.

Mkuu wa Idara ya Uchumi FCT, Kulwa Msogoti, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akiwasilisha mada ya majukumu yanayotekelezwa na baraza hilo kwenye semina ya wadau wa mkoa wa Dodoma.

Alisema mashauri hao yaliyoshughulikiwa ni sawa na asilimia 97.1 huku mashauri 13 yakiwa kwenye hatua mbalimbali za usikilizwaji.

"Katika mashauri yaliyopokewa, masuala ya nishati na maji ndiyo yanayoongoza kwa kuwa tulipokea mashauri 174 na tayari 168 yameamuliwa na yamebaki sita ambayo yako hatua za usikilizwaji," alisema.

Akifungua semina hiyo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Kaspar Mmuya, alipongeza baraza hilo kwa kutoa elimu itakayowasaidia Watanzania kwenye biashara kwa kuongeza kasi ya uwajibikaji ili kujiepusha na migogoro ya kiushindani.

"Serikali imeweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara na wawekezaji kwa kuunda chombo hiki na Rais Samia Suluhu Hassan ametoa nafasi kupitia FCT kutoa maoni ili kudhibiti soko na ushindani na kuleta usawa,"amesema.

Naye Kaimu Msajili wa Baraza hilo, Kunda Mkenda, alisema elimu inayotolewa na FCT ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake kisheria kwa kuwa ni chombo cha rufaa kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 83(1) cha Sheria ya Ushindani namba nane ya Mwaka 2003.

Alisema lengo la kukutana na wadau hao ni kukuza na kulinda ushindani wa kibiashara na kumlinda mtumiaji wa bidhaa.

Ofisa Sheria Mkuu wa FCT, Hafsa Said, alisema mashauri hayo yamekuwa yakiamuliwa ndani ya miezi sita na kwa sasa baraza linaboresha mazingira ya kuwafikia wadau ili kusajili mashauri kwa njia ya mtandao.

"Baraza linaendesha mashauri kama mahakama lakini kiutendaji liko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwa sasa tumefanya mapitio ya Sheria ya Ushindani na tuko kwenye mchakato wa kupitia kanuni ili ziendane na wakati kwa kuwa zimekuwa za muda mrefu tangu mwaka 2012.

Washiriki wa semina hiyo, Faustine Mwakalinga na Grace Onea walipongeza baraza kwa kutoa elimu hiyo na kushauri kuendelea kukutana na wadau kwa kuwa wengi bado hawajajua majukumu na umuhimu wa FCT ili kuepuka migogoro ya kiushindani.




Waziri wa Madini, Antony Mavunde (kulia), akikata utepe kuzindua gari la wagonjwa 'Ambulance', lililokabidhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamini Mkapa, jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Kaspar Muya. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Uzalishaji maji safi, salama waongezeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa ripoti ya utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2022/23 iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imebainisha kuwapo na ongezeko la uzalishaji wa maji kwa lita bilioni saba sawa na asilimia 1.78.

Akiwasilisha bungeni juzi utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2024/25, Waziri Jumaa Aweso, alisema taarifa hiyo imeonyesha pia kuongezeka kwa uwezo wa miundombinu ya kuzalisha maji kwa lita bilioni 126 sawa na asilimia 16.94 na kuongezeka kwa idadi ya wateja wanaopata huduma ya maji kwa asilimia 11.

Hata hivyo, alisema taarifa imebainisha changamoto zinazokabili mamlaka za maji zikiwamo kuongezeka kwa upotevu wa maji ambao umefikia asilimia 37, upungufu wa miundombinu ya huduma ya usafi wa mazingira na uwiano usioridhisha wa ongezeko la mahitaji ya maji ikilinganishwa na uzalishaji wa maji.

Aweso alifafanua kuwa huduma za maji mijini zinadhibitiwa na EWURA kupitia Kifungu namba 414 cha Sheria Na.11 ya EWURA ya mwaka 2001.

"Sheria hiyo inaitaka EWURA kudhibiti utoaji wa huduma kwenye Sekta za Maji na Nishati katika maeneo ya maji na usafi wa mazingira, umeme, mafuta ya petroli pamoja na gesi asilia,"alisema.

Alieleza kuwa majukumu ya EWURA ni pamoja na kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao.

"Hadi mwezi Aprili 2024, EWURA ilitoa leseni nne za kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji ya Rombo, KyelaKasumulu, Njombe na Busega," alisema.

Kadhalika, alisema EWURA ilitathmini na kuidhinisha bei mpya za huduma ya maji kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira saba ambazo ni Dodoma, Makonde, Sumbawanga, Orkesumet, Mombo, Bariadi na Lindi.

Pia alisema katika kipindi hicho, EWURA ilifanya mapitio ya mipango biashara ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 11 na kuidhinisha mikataba sita ya huduma kwa mteja kwa mamlaka za Musoma, Liwale, Makambako, Lindi, Biharamulo na Geita.



## Kampuni uzalishaji vifaranga yabanwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Zanzibar Marine Hatchery inayojishughulisha na uzalishaji wa mazao ya baharini iliyoko Beit El Ras visiwani hapa, imetakiwa ndani ya miezi miwili kuleta matokea ya uzalishaji wa vifaranga vya majongoo bahari ili kuleta mafanikio kwa wafugaji na serikali.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika kituo hicho na kutoridhishwa na hali ya uzalishaji.

Waziri Shaaban alisema serikali ina nia njema na mwekezaji huyo katika kuiendesha 'hatchery' ili kuleta kuleta matokeo yaliotarajiwa na serikali kwa kiwango kikubwa.

"Niseme wazi sijaridhika na uendeshaji wa kituo hiki cha kutotoleshea vifaranga si mzuri na nitachukua hatua kwenye eneo la Hachery"alisemwa waziri huyo.

Aidha alsiema hatchery hiyo imekua na malalamiko makubwa ambayo yanahitaji kuchukuliwa hatua kutokana na uongozi uliopo umegawa matabaka ya watendaji wa Kampuni na waserikali jambo ambalo linaleta changamoto kwa wasimamizi wa kituo na watendaji.

Shabaani alsiema lengo serikali kuunga ubia na Kampuni hiyo kuwa pamoja na watumishi wa serikali ili kuwarithisha utaalamu wa uzalishaji wa vifaranga kwa watumishi hao.

Naye Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Sheha Idrisa Hamdani, alisema agizo la Waziri amelipokea na watalifanyia kazi kwa muda sahihi waliokubaliana na uzalishaji wa vifaranga vya majongoo bahari katika kituo hicho.

Wakati huo huo, waziri huyo alitembelea Kampuni ya Zanz International iliyoko Mtoni Unguja inayojishuhulisha na usafirishaji wa kaa nje ya nchi na kuweka bayana kuwa kituo hicho hakijaleta matokea ya uwekezaji hadi sasa.

**"Niseme wazi sijaridhika na uendeshaji wa kituo hiki cha kutotoleshea vifaranga si mzuri na nitachukua hatua kwenye eneo la Hachery"alisemwa waziri huyo.**

# Mfumuko wa bei wapungua Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KASI ya mfumuko wa bei kwa mwaka kutoka Aprili 2023 hadi Aprili 2024, imepungua kufikia asilimia 4.88 kutoka asilimia 4.92 iliyorekodiwa Machi, mwaka huu pekee.

Mkuu wa Takwimu za Bei Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Hassan Jamal Hassan, alisema jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa Habari, Mazizini, nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema bidhaa zilizosababisha kupungua kwa mfumko wa bei na asilimia kwenye mabano ni mchele wa Mbeya (11.5), unga wa ngano (3.0), unga wa sembe (7.5), mafuta ya kupikia OKI (5.6), ndizi za mkono mmoja (21.3) na ndizi za mtwike (30.4).

Alisema kwa ujumla faharisi za bei zimeongezeka na kufikia 111.42 kwa mwezi Aprili 2024 ikilinganishwa na 106.24 ambayo iliripotiwa katika mwezi kama huo mwaka jana.

Hassan alisema kundi la bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kileo kwa Aprili, 2024 zimeongezeka na kufikia asilimia 7.82 ikilinganishwa na asilimia 7.38 iliyorikodiwa katika mwezi wa Machi 2024.

Kwa upande wa mfumuko wa bei Aprili, mwaka huu, umeongezeka na kufikia asilimia 1.81 ikilinganishwa na asilimia hasi 0.09 iliyorikodiwa katika kipinjdi kama hicho, mwaka jana.

Pia alisema mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kileo kwa Aprili, 2024 umeongezeka na kufikia asilimia 3.80 ikilinganishwa na asilimia hasi 0.51 iliyorikodiwa katika Machi, mwaka huu.

Meneja Msaidizi - Uchumi Benki Kuu ya Tanzania (BOT) Tawi la Zanzibar, Shamy Chamicha, alisema kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei ni hatua nzuri ya kiuchumi na malengo yaliokuwepo ya kubakia kwenye tarakimu moja.

"Ni ahueni kwa wananchi na hii inatokana na kuwepo kwa bidhaa za kutosha kwenye masoko. Lakini kwa ujumla hali ya uchumi imeendelea kubakia vizuri na hata upatikanaji wa dola hivi sasa upo vizuri," alisema.

Mfumuko wa bei wa Zanzibar ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazokusanywa katika masoko ya miji ya Zanzibar.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani (katikati), akipata maelezo kuhusu maboresho ya Bandari ya Tanga kutoka kwa Kaimu Meneja wa Bandari hiyo, Peter Milanzi (kulia), alipotembelea bandarini, jijini Tanga jana. Kushoto ni Katibu Tawala wa Mkoa huo, Pili Mnyema. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wataalamu ujenzi kuwezeshwa maarifa zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitaendelea kuweka mazingira mazuri kwa kuziimarisha taasisi za ujenzi ili kuhakikisha wataalamu wazawa wanakuza taaluma zao na kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa miradi inayojengwa na Watanzania.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwaendeleza wataalamu wa usanifu, uhandisi na wakadiriaji majengo Tanzania katika Viwanja vya Maonyesho Nyamanzi, nje kidogo ya Zanzibar.

Hemed alisema serikali zote mbili zimetoa kipaumbele kwa wataalamu wa ujenzi na kampuni za ndani kupitia wizara na taasisi ambazo zimefanya jitihada maalum za kuweka sera, sheria na kanuni zenye vigezo rafiki ili kurahisisha maombi ya kazi za ujenzi nchini.

Makamu wa Pili wa Rais pia aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuitumia vyema nafasi waliyoipata ili kupata uwelewa mkubwa na mbinu za ujenzi ikiwamo utumiaji wa njia mbadala ya vyuma hasa Zanzibar ambako kumekuwa na uhaba mkubwa wa matumizi ya mali zisizorejesheka kama vile mchanga.

Alisema matumaini makubwa ya serikali kuwa mafunzo hayo yatasaidia kuonyesha mbinu za kuhifadhi, kuitunza na kuiendeleza miji ya urithi ambayo inachangia kuongeza pato la taifa kupitia watalii wanaofika nchini.

Hata hivyo aliyataka Makampuni na wataalamu wa ujenzi kuendelea kuwa waadilifu katika kutekeleza majukumu yao ikiwamo kuzingatia ubora unaohitajika na muda wa mradi uliopangwa ili kutumika kama ilivyokusudiwa na kudumu kwa muda mrefu kwa faida ya vizazi vya sasa na baadae.

Akiwasilisha taarifa ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiano na uchukuzi, Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk Mngereza Mzee Miraji, alisema kufanyika kwa mafunzo hayo kunatokana na ushirikiano uliopo kwa pande mbili za Muungano kuhakikisha kunakuwa na wataalamu wabobevu hasa katika masuala ya kutunza na kuboresha miji ya urithi wa dunia.

Dk. Mngereza alisema ushirikiano uliopo katika sekta za ujenzi kwa Tanzania Bara na Zanzibar umesaidia kuimarika kwa miundombinu ya barabara na kusababisha kuongezeka kwa kipato kwa mwananchi na taifa pamoja na kuimarika kwa huduma za kijamii.

Wenyeviti wa bodi za usajili wasanifu, wahandisi na wakadiriaji majengo kutoka Zanzibar na Tanzania Bara, walizishauri serikali kutumia wataalamu wazalendo katika shughuli za ujenzi ili majengo na miji ya urithi yawe bora zaidi.

Pia walisema wakati umefika kwa serikali kuangalia sheria na miongozo katika masuala ya ujenzi ili kupunguza changamoto ya kujengwa kwa majengo yasiokidhi viwango na ubora na kuendelea kulitia hasara taifa.



**RAYVANNY**

UKURASA 13



Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



# SHAMSA NI WEWE?

SIKU chache zilizopita msanii mkongwe wa filamu za Bongo Muvi, Shamsa Ford, amejianika hadharani kuwa yeye ni mjamzito.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Shamsa ameweka picha akiwa amevaa nguo ya rangi nyeupe iliyoachia mbele na kuonyesha wazi tumbo lake.

Hatua ya kuonyesha ujauzito katika mtindo wanaofanya mastaa wengi kuweka wazi eneo la mbele la tumbo, imesababisha baadhi ya mashabiki wake kughadhabika kwa kile walichosema kutokana na umri wake hakupaswa kufanya hivyo.

Idadi kubwa ya watu waliochangia maoni picha hiyo, wamesema kutokana na umri na jinsi anavyojiweka hakustaili kuweka picha ya aina hiyo kwani sawa na kujianika hadharani.

Shabiki mmoja anayefahamika Reb4385 ameandika "Kwa staha yako umejiaibisha kufanya namna hivi,"

Huruma Sigala, yeye amehoji "Ameanzaje hayo mambo Shamsa jamaniii?

BASI SAWA

## Abbah apigilia msumari mwingine



VITA kati ya watayarishaji wawili maarufu wa muziki wa Bongo Fleva, Abbah Process na S2Kizy imeingia katika sura mpya, baada ya Abbah kueleza kwamba kazi yake moja ni sawa na nyimbo 10 za mpinzani wake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Abbah ameandika kwamba nyimbo 50 alizofanya S2Kizy ni sawa na zake 10 ambazo zinamnyima usingizi kwa sasa.

"Ninachomaanisha hapo kuwa wimbo wangu mmoja sawa na zake nyingi, natoa midundo ya milele lakini yeye anatoa 'bubble Gum' (bazooka). Sitaongea tena naomba mniamini," amesema Abbah.

## Diamond, Zuchu kwa raha zao



WANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz na Zuchu, wamewaacha midomo wazi mashabiki wao baada ya kuonekana wakiwa pamoja katika hisia kali za kimahaba.

Wasanii hao kila mmoja aliweka kipande cha video ikiwaonyesha wawili hao wakiimba wimbo wao mpya unaoitwa raha, katika hali ya kimahaba na kuashiria kwa sasa wamemaliza tofauti zao.

Zuchu na Diamond hivi karibuni walionekana kuwa tofauti na kusababisha kuwepo kwa tetesi kwamba wanamuziki hao ambao wapo katika uhusiano wa kimapenzi wameachana.



## RAYVANNY SUKARI YA WAREMBO

TUKIO la mwanamuziki wa Bongo Fleva nchini, Reyvanny kusimamisha shoo yake kwa muda baada ya warembo kuvamia jukwaa limekuwa na maoni tofauti.

Katika shoo yake kubwa iliyofanyika nchini Burundi hivi karibuni, Rayvanny alijikuta katika wakati mgumu baada ya warembo kuvamia jukwaa na kwenda kumkumbatia huku wengine wakiangua kilio kutokana na mahaba naye.

Baadhi ya watu walioshiriki kutoa maoni katika video hiyo, wamesema kitendo hicho kinaonyesha jinsi gani Rayvanny alivyokuwa mkubwa kisanii tofauti na watu wengine wanavyomuona.



## Vera usikasirike lakini....

MPAMBAJI wa video za wanamuziki kutoka Kenya, Vera Sidika, amesema angetaka kuwa na watoto wazuri ana uwezo wa kwenda kununua mbegu za kiume hospitali.

Vera amesema hayo baada ya mtu mmoja kutaka maelezo kwa nini alichana na Mauzo, au kwa sababu tu alitaka kupata watoto wenye sura nzuri.

"Kama ni jeni nzuri hadi benki ya mbegu za kiume ziko, kwa kweli unaweza hata kuchagua rangi ya macho unayotaka mtoto wako awe nayo." Amesema Vera

FILAMU

## Simbinlani Shujaa: Haramu kwako, halali kwetu

**Na Adam Fungamwango**

SIMBINLANI Shujaa ni filamu inayotufundisha kila mmoja kuheshimu hisia za mwenzake. Kuna kitu ambacho kwako kinaweza kuwa si kizuri, lakini kwa mwenzako hakina tatizo, basi mwache tu. Haiwezekani kitu ambacho kwako hukipendi, basi ulazimishe watu wote wakikatae kama wewe.

Imechezwa na wasanii Anita Ngereza, Agnes Makalla, Ayoub Kinyamagoha, Jesco Maryego, Madaraka Manase, Enea Msukwa, Haidari Mlingo, Sakina Njoka na wengineo

Ndani ya himaya fulani, mfalme anafariki. Baada ya msiba kumalizika anamuachia urithi kijana wake wa kiume.

Tofauti na baba yake aliyetawala kwa busara, mfalme huyo kijana anatawala kwa mkono wa chuma.

Wananchi hawana amani. Kwenye himaya hiyo kuna kijana mmoja aitwaye Simbi. Ni kijana mwenye nguvu, busara na anayependwa na wengi. Dada wa mfalme kijana anatokea kumpenda Simbi. Awali Simbi alikataa. Lakini alipotaka kujiua akakubali. Penzi halijaribiwi. Simbi akaanza kumpenda zao.

Penzi halina siri na siri si ya watu wawili, Mfalme akagundua. Akampiga mkwara dada yake asiendelee kuwa na mahusiano na Simbi, kwani ni kijana wa kimasikini na dhalili. Akamwambia atamuozesha kwenye himaya nyingine ya mfalme. Zao akakataa. Akamwambia moyo wake uko kwa Simbi.

Kijana mfalme akaamua kuitesa familia ya Simbi pamoja na yeye mwenyewe. Kazi yake ikawa ni kutuma walinzi wake watiifu kwenda kutesa dada za Simbi, pamoja na yeye mwenyewe.

Hali ilizidi kuwa mbaya, lakini Zao na Simbi hawakuacha kupendana. Ilikuwa ni kama kumpigia gitaa mbuzi.

Mfalme naye hakukoma, aliwaandama kweli kweli. Dada wa mfalme uzalendo ulimshinda na kuamua kujiua. Lilikuwa pigo kubwa kwa mfalme. Kwa hasira akawasingizia Simbi na dada zake wawili ndiyo waliosababisha dada yake ajiue. Pamoja wazee wa kimila kudai hakuna ushahidi wa kuwatia hatiani, mfalme hakuridhika, akataka kuwaua mwenyewe kwa upanga wake.

Ndipo mzimu wa dada yake, Zao ulipotokea wakati panga lipo juu kutaka kukata kichwa cha Simbi, ukazuia. Mfalme alichanganyikiwa na kukubali kuwa alifanya makosa kutosikiliza hisia za dada yake.




## PICHA 5 KALI ZILIZOTIKISA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE miaka ya 1980, hadi katikati ya miaka ya 1990, kabla ya televisheni kuenea majumbani kuanzia katikati ya miaka ya 1990, vijana na watoto wengi walikuwa wakienda maeneo mbalimbali ili kuona sinema.

Wengine walienda kwenye majumba makubwa ya sinema. Hao ni kwa wale kwenye uwezo. Wengine walikwenda maeneo ambayo yalikuwa yana afadhali kidogo. Lakini wengi wao hasa watoto walikuwa wakienda kwenye sehemu ambazo kwa sasa zinaitwa 'vibanda umiza'.

Huko utakuta mtu kazungushia tu magunia na ndani kaweka televisheni yake, akionyesha filamu mbalimbali.

Achilia mbali filamu za Kichina, ambazo nyingi ni za sanaa za mapigano, na kihindi ambazo tutakuja leo tutaziangalia filamu za kizungu.

Kulikuwa na filamu nyingi maarufu za kizungu ambazo hakuna kijana au mtoto ambaye alitaka kuzikosa. Leo tunakwenda kuangalia filamu hizo.

### War Bus

Ni filamu maarufu sana kwa Wabongo, ambayo ilitoka mwaka 1985. Mastaa wa picha hii ni Daniel Stephen, Romano Kristoff na Urs Althaus.

Msingi wa picha hii ni vita ya Vietnam. Ni makomandoo watatu wa Kimarekani waliokwenda kuwaokoa mateka walioshikiliwa na 'wavete', kama walivyokuwa wakiitwa watoto wakati huo.

Kilichovutia zaidi watazamaji wengi wa filamu hiyo, siyo operesheni hiyo, bali ni staili ya makomandoo hao ambao waliamua kuteka basi ya shule na kulitumia kama usafiri wa kwenda kuwaokolea watu wao. Ile staili ya ulinzi wa mmoja kukaa mbele ya boneti la basi, mwingine juu kwa ajili ya ulinzi, mwingine ndani, pamoja na mbwembwe zao, ndiyo msingi wa picha hii kupendwa.

### American Ninja

Hii pia ni filamu ambayo iliwanyima watu usingizi, ikitoka mwaka 1985 kama 'War Bus'.

Wakubwa, vijana na watoto wa Kibongo waliipenda sana filamu hii, ikimhusisha staa mmoja anaitwa Michael Dudikoff. Huyu ni askari wa Kimarekani ambaye pia ana ujuzi mwingine wa kupigana na watu wanaitwa maninja, ujuzi alioupata akiwa mdogo.

Humu anatwangana na maninja kisawasawa na kuwashinda, kiasi cha kuwa moja ya filamu bora sana na kukumbukwa hadi leo.

### No reareat, no surrender

Filamu hii ilitoka mwaka 1986. Hii siyo ya kivita kama 'War Bus'. Wala siyo ya mapanga na sanaa za kininja. Picha hili ni la sanaa wa mapigano. Humo ndano zimepigwa balaa. Stelingi kwenye filamu huu ni staa aliyekuwa maarufu sana wakati huo, Jean Claude van Damme. Huyu alisifika sana kwa mateke ambayo ndiyo yaliyokuwa yanampa zaidi ushindi. Ni moja kati ya filamu maarufu na iliyopendwa sana.

### Komando Kipensi

Jina halisi ya picha hili ni 'Deadly Pray'. Lakini nadhani hadi leo si wengi wanaojua jina halisi ya filamu hii. Lakini ukiwaambia 'Komando kipensi', kila mtu atasema anaifahamu.

Sidhani kama kuna mtoto au kijana wa miaka ya 1980 mpaka 2000, ambaye haifahamu filamu hii. Ilitoka mwaka 1987.

Jamaa anaitwa Troy Donahue, au kwa jina la picha ni Mike Danton. Huyu ni jeshi la mtu mmoja. Anapigana akiwa amevaa pensi tu, ndiyo maana wakamwita hivyo. Alimchokoza wenyewe. Walikuwa hawajui kuwa ni mwanajeshi mstaafu. Walitaka kumfanya chambo. Ikawa ni vita vya ajabu.

### Delta Force

Ilitoka mwaka 1986. Ni moja kati ya filamu maarufu sana kwa Wabongo wakati huo. Staa wa filamu hii ni mkongwe Chuck Norris. Ni picha la kivita.



# Mpho Sebeng afariki dunia

MWIGIZAJI mkongwe wa Afrika Kusini, Mpho Sebeng, amefariki dunia.

Kulingana na familia yake, msanii huyo wa filamu alifariki Mei 5, baada ya kupata ajali ya gari katika eneo la Potchefstroom katika jimbo la North West.

"Familia ya msanii wa uigizaji wa Afrika Kusini, Mpho Sebeng, kwa majonzi tunathibitisha kwa umma kuwa mtoto wetu ameaga dunia," ilieleza taarifa ya familia hiyo.



## Nasboi huo ni utovu wa nidhamu

MWANAMUZIKi kutoka Nigeria, Nasboi ameweka wazi kwamba hahitaji ruhusa kutoka kwa wazazi wake kuoa mwanamke anayempenda.

Katika mazungumzo yake hivi karibuni, mwimbaji huyo alieleza kwa nini anaweza kufunga ndoa na mwanamke hata kama mama yake hajamkubali.

Amesema katika historia ya familia yake haina tatizo la ukabila na anaweza kukutana na kupanga ndoa na mwanamke anayempenda bila kupata ruhusa ya wazazi.


## Skales una wanawake 100?

RAPA maarufu wa Nigeria, Skales, amesema amekuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanawake zaidi ya 100, na kujifananisha na Mfalme Suleiman aliyetajwa katika kitabu cha Biblia.

"Nimetoka kimapenzi na wanawake wapatao 100 hivi. Kama nisingeoa labda ningekuwa kwenye njia ya Mfalme Suleiman," amesema wakati akihojiwa na radio moja.

Katika Biblia inaeleza mfalme Suleiman alikuwa na wake 700 na masuria 300.





## Aliyemjeruhi mlinzi wa Drake asakwa

TUKIO ufyatuaji risasi karibu na jumba la kifahari la rapa maarufu nchini Marekani, Drake, limeibua hali ya wasiwasi kuhusu usalama wa maisha ya msanii huyo.

Ripoti zinasema mtu mwenye silaha alifika katika eneo lililojengwa jumba hilo linaloitwa Toronto katika kitongoji cha Bridle Path na kumlenga mlinzi wa rapa huyo kwa kumpiga risasi na kumjeruhi vibaya.

Ingawa haijafahamika iwapo Drake alikuwepo wakati wa tukio hilo, vyanzo vinaeleza kuwa mwanamuziki huyo anashirikiana na polisi katika uchunguzi wa tukio hilo.

Mtu huyo alitoweka mara alipofanya tukio hilo na polisi wametangaza kufanya msako wa kumtafuta.

## Davido asherehekea kujaza Wembley

MKALI wa Afrobeats, David Adeleke, maarufu kama Davido, amekuwa na furaha baada ya kuingia kwenye rekodi ya wasanii wa Nigeria waliofanikiwa kujaza watu katika uwanja wa Wembley, nchini Uingereza.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Davido amewapongeza mashabiki zake waliokwenda kwenye onyesho lake na hatimaye kuujaza uwanja huo wenye uwezo wa kuingiza watu 90,000 kwa mara moja.

Mwimbaji huyo mwenye mafanikio kwa miaka 12, amesema kwa mafanikio hayo sasa amejiunga na wasanii kama Burna Boy na Wizkid ambao walifanikiwa kuujaza katika maonyesho yao.



## Madiwani wataka kusitishwa haraka ugawaji mashamba

**Na Steven William,** MUHEZA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, wametaka kusitishwa haraka kwa ugawaji wa mashamba kwa shughuli mbalimbali kwa wawekezaji 28 walioomba mpaka upatikane mwafaka.

Hayo yalitokea juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri chini ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina na kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Cyprian Mselem.

Madiwani hao walimwagiza mwenyekiti asitie Saini muhtasari wa Agosti 24, mwaka jana wa makubaliano ya wawekezaji hao kupewa ardhi katika wilaya hiyo kwa kuwa una makosa na utawatia katika matatizo wawakilishi hao wa wananchi.

Pia waliagiza wawekezaji waliopatiwa maeneo hayo kwa shughuli mbalimbali ambao wanaendelea hivi sasa waandikiwe barua ya kusitisha shughuli zao mpaka mwafaka utakapofikiwa kati yao na madiwani kufuata utaratibu upya wa kuomba maeneo.

"Tunaagiza mwenyekiti usitie saini muhtasari huo wa makubaliano ya wawekezaji kupatiwa ardhi kwa shughuli mbalimbali utatuletea matatizo sisi madiwani hapo baadaye kwa kuwa hatukushirikishwa katika ugawaji wa mashamba hayo kwa wawekezaji," alisema Diwani wa Makole, Shabani Achimwene.

Diwani wa Magila, David Kilua, aliibua hoja hiyo alipouliza swali katika muhtasari wa kamati ya Uchumi, ujenzi na mazingira wa Oktoba 19, mwaka jana, kuwa ni taratibu gani zilizotumika kugawa ardhi kwa wawekezaji katika sekta mbalimbali.

Kutokana na swali hilo, hoja hiyo iliibua mjadala na kuungwa mkono na Diwani Achimwene, Diwani wa Kisiwani, Shabani Chewaja, na madiwani wote, uliodumu takribani saa mbili.

Akijibu hoja za madiwani, Mhina alisema taratibu zilizotumika kuwapata wawekezaji hao ni zile walizokubaliana katika kikao cha baraza la Madiwani Agosti 24, na kuthibitishwa na baraza la madiwani

Diwani wa Kicheba, Hamisi Mkodingo, alisema ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji umeshaingia shaka kwa madiwani, hivyo mchakato uanze upya na kutupilia mbali ule wa zaman. Hoja hiyo iliungwa mkono na Diwani wa Kwafungo, Gabriel Mswagala, Diwani wa Kilulu, Fuad Rashid na Diwani wa Genge Moses Kisiki.

# Wataalamu afya ya akili wataka sera kudhibiti wanafunzi kukariri

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WATAALAM wa afya ya akili, wameishauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuandaa mpango maalum wa kisera, utakaowadhibiti walimu wa shule za msingi na sekondari kutowalazimisha wanafunzi kukariri silabasi fulani kwenye masomo ili kuisaidia shule kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa.

Daktari bingwa wa afya ya akili wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, Aloyce Ambokile, alisema baadhi ya walimu hawatumii kanuni za kisaikolojia, badala yake wanatumia nguvu kubwa ya kuchapa viboko, kitu ambacho kinaathiri afya ya akili.

Dk. Ambokile alikuwa akizungumza jana katika kongamano la mwaka la utendaji wa mashirika ya kiraia.

"Wako wanafunzi wanaochapwa ili kulazimishwa kuelewa masomo fulani, jambo ambalo siyo sahihi. Kwa kuwa wanapaswa kujengwa kisaikolojia na siyo kulazimishwa.

"Mtu anafanya vibaya shuleni, halafu watu wanachapa tu wakati anatatizika kwenye akili. Kuna wenye tatizo la namba (hesabu) Sasa matokeo ya kulazimishwa, ni kuanza kufeli masomo mengine mfano Jiografia, Fizikia, Kemia, Biolojia na mengine. Lakini kumbe angepelekwa kwenye kituo cha huduma angepata tiba ya kisaikolojia," alisema Dk. Ambokile.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Charles Mkombachepa, aliwataka wananchi kutokuwanyanyapaa wagonjwa wa akili na kuwaita majina yanayoonesha kuwatenga na badala yake wawahimize kwenda Vituo vya kutolea huduma Ili waweze kupatiwa matibabu.

"Nitoe rai kwa wananchi tusiwanyanyapae wagonjwa wa akili Kwa kuwaita vichaa, chizi, tahira hii inawafanya wajitenge na kujiona hawafai na hata wakupata Ushauri wa kwenda kwenye matibabu hawakubali.

Kwa kuwa wanahisi wataenda kuitwa majina hayo hayo, ni vyema tukawatia moyo na kuwaelekeza sehemu sahihi za kwenda kupata matibabu," alisema.

Alisema mkoa wa Arusha una vituo vingi vya kutolea huduma ya afya ya akili ikiwamo Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, Kituo cha Afya Levolosi na Hospitali ya Wilaya ya Longido.

Katika kongamano hilo, Mkurugenzi wa Shirika la Self Awareness for Every one (SAFE), Julieth Kiswaga, alisema matatizo ya akili husababisha mtu mmoja kati ya 100 kufariki dunia.

Kwa mujibu wa Kiswaga, utafiti uliofanywa na wataalamu wa afya ya akili duniani, ilibainika kuwa kila watu wanane, mmoja ana tatizo la afya ya akili.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Mental Health Tanzania, Onesmo Petro, alisema lengo la kuandaa kongamano hilo,ni kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu afya ya akili na kuondokana na unyanyapaa katika jamii.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, Anjelina Marko (kushoto), akipokea majarida mbalimbali kutoka kwa Meneja Miradi wa Shirika la Frankfrut Zoological Society (FZS), Masigeri Rurai, wakati wa ufunguzi wa ofisi ya Kidijitali ya kudhibiti wanyamapori waharibifu wilayani humo, juzi. Katikati ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Bwenda Ismael na (kulia) ni Ofisa Uhusiano wa taasisi hiyo, Samira Papillon. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makonda aweka msimamo kuhusu madaraka

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amesema kuwa yuko tayari kupoteza wadhifa huo,kwa kuwa atasimama bega kwa bega kuwatetea wananchi waliopokwa haki kimabavu na watu wenye uwezo wa kifedha na watendaji serikalini ili wapate haki zao.

Makonda alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati wa kliniki maalum ya kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili wananchi na asilimia kubwa zilikuwa za migogoro ya ardhi, kudhulumiwa nyumba, mafao kwa wastaafu na mirathi.

Aidha, alisema wadhifa na cheo chake hakitakuwa na faida kwake endapo atashindwa kuwasaidia wananchi wa mkoa huo, waliodhulumiwa na watu wenye vyeo na nguvu ya kifedha kupata haki zao.

"Wako baadhi ya watendaji serikalini wanaowasilikiza watu kutokana na kipato chao kwa kuwa msingi wa uongozi wowote au taasisi ni haki na pale inapokosekana kunakuwapo na majonzi,maumivu,kukata tamaa,ugomvi na vita na wakati mwingine watu wanapoteza maisha.

"Kwa kiwango kikubwa wanaofanya hayo sio wananchi bali ni sisi watendaji na rushwa ni adui wa haki kwa kuwa jamii inayoongoza kwa ruswa ni jamii isiyotoa haki na tuna tamani mkoa huu uwe mfano kwa kumthamini mtu na utu wake ili kupunguza maumivu ya wananchi," alisema.

Mkonda alisema katika kliniki hiyo,kutakuwa na chemba 75 na mabanda 23 ambapo kwenye kila banda kutakuwapo na mwanasheria wa kujitegemea wakishirikiana na wa Serikali na huduma itatolewa bure kwa wananchi kwa siku tatu kuanzia Mei 8 mpaka 10.

"Tumeamua kila banda tutamchomeka mwanasheria mmoja wa kujitegemea kwenye kila idara ili wakawe watu wa upande wa pili wa kusikiliza na kuangalia kama watendaji wa serikali wanatenda haki.

"Ninaomba wananchi msikubali kutoka kwenye dawati bila ya kuridhika na kupata haki yako yote iliyokamilika iwe mbivu au mbichi ni lazima upambane kuhakikisha unapata haki yako.

"Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, tangu mwanzo alishajipambanua kuwa hataki mali ya dhuluma hivyo na kwa watumishi wa serikali tusiwadhulumu wala kutumia nafasi zetu kuwakandamiza wananchi," alisema.

Honorata Temu, alisema yeye ni mjane alifiwa na mume wake mwaka 1984 akiwa kazini na alifuata utaratibu wa kisheria kwa kipindi chote kudai malipo ya fidia lakini hakusaidiwa.

"Nimezunguka kwenye ofisi mbalimbali za serikali nikiwa na nyaraka muhimu lakini mpaka sasa imepita miaka mingi bado sijapata haki ya kulipwa mirathi ya fidia ya malipo ya mume wangu kufia kazini," alisema.

Shedrack Letioni, mkazi wa Mtaa wa Lemara Kati, alisema wamedhulumiwa na ndugu yao shamba ambalo lilikuwa la familia lililoachwa na baba yao.

"Tulikwenda kwa wazee wa ukoo walitupeleka ofisi ya kata na lilikwenda kugawanywa shamba lile na kila mwanafamilia akigawiwa eneo lenye upana wa mita 25 na urefu mita 261 lakini baada ya hapo, ndugu yetu aliendelea kung'ang'ania shamba hilo.

Dina Nnko, alisema baada ya mume kufariki dunia, ndugu wa marehemu walimnyang'anya mali ikiwamo nyumba ambayo anategemea kuishi na watoto wake.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Unajua Marijani, Maneti, Bitchuka walicheza soka?



Marijan Rajabu



Hemed Manet

**Na Adam Fungamwango**

HIVI usingekuwa na kazi unayoifanya sasa, ungefanya shughuli gani?

Hili ni swali linaloulizwa sana au ambalo wewe mwenyewe unajiuliza.

Mfano daktari anajiuliza kama asingekuwa hivyo angefanya kazi gani?

Wengine wanaweza kuonekana na kipaji fulani, lakini baadaye akaangukia kwenye kipaji kingine kabisa na kukiacha kile cha mwanzo hadi watu wakashangaa.

Leo nakuletea mfano wa wanamuziki watatu wakubwa tu nchini ambao walikuwa wanamuziki maarufu sana, lakini kabla ya kuwa hivyo walikuwa wacheza soka wazuri kiasi kwamba awali walitabiriwa kuwa wanaweza kuchezea hata klabu kubwa nchini za Simba na Yanga.

Nikisema hivyo nina maana halisi kuwa walicheza kwa kiwango cha juu sana.

Hao ni Marijani Rajab, Hemed Maneti na Hassan Bitchuka. Leo sitaki kuwaeleza sana kuhusu kazi zao za muziki, ila yale ambayo wengi hawayafahamu.

Marijani, aliyezaliwa Machi 23, 1955 na kufariki mwaka 1995, aliondokea kuwa mwanamuziki mkubwa nchini ambaye hata watoto wanaokuwa leo wanakuja kukuta jina lake 'likiimbwa', pamoja na nyimbo zake kama 'Georgina', 'Siwema', 'Zuwena,' 'Hanifa', na nyingine nyingi.

Kifupi ni kwamba Marijani alikuwa mwanamuziki wa bendi ya STC, Safari Trippers na Dar International. Alizaliwa Dar es Salaam maeneo ya Kariakoo. Alikuwa mtoto wa mjini haswa.

Mbali wakati anaanza muziki, alikuwa pia ni golikipa mzuri mno. Alizidakia timu mbalimbali Karikaoo na Ilala, ikiwemo timu maarufu ya Kahe FC. Kuna wakati alikuwa akitoka kucheza mpira, anaoga na kwenda dansini. Alishaanza pia kudakia timu ya vijana wa Simba. Kutokana na mahaba yake na klabu ya hiyo, wengi walitarajia kuwa angekuja kuwa kipa wa klabu ya Simba. Hata hivyo kwa kauli yake mwenyewe akiwa hai ni kwamba, sauti ya muziki, iliizidi ya soka, akawa mwanamuziki.

Mwingine ni Hemed Maneti. Mwanamuziki mwimbaji wa bendi za Cuban Marimba, TP Limpopo za Morogoro, na Vijana Jazz. Alifariki Mei 31, 1990 kwenye Hospitali ya Mwananyamala, Dar es Salaam.

Mbali na kuimba na kutunga nyingi nyingi, Maneti aliyezaliwa Muheza Tanga, alikuwa pia mcheza soka mahiri.

Huenda kama asingekuwa mwanamuziki angekuwa mchezaji mzuri kama ambavyo angekuwa Marijani.

Historia inasema kuwa aliwahi kucheza timu moja ya Omari Gumbo ambaye baadaye alikuwa winga hatari wa klabu ya Simba, lakini pia akaiongoza klabu hiyo ya Msimbazi.

Lakini waliachana, Gumbo akaendea na mpira, Maneti kwa kuwa alikuwa pia na kipaji ya muziki, akaendelea nacho. Haijajulikana Maneti alikuwa shabiki wa timu gani.

Mtoto wake aitwaye Maneti Hemed alichukua kipaji cha soka cha baba yake na kuchezea klabu mbalimbali, Dar es Salaam, ingawa hakubahatika kuchezea klabu kubwa.

Mwingine ni Bitchuka. Huyu kwa bahati nzuri yupo hadi leo. Pamoja na kuwa mwimbaji mwenye sauti nyororo, akizipigia bendi karibuni zote kubwa nchini, Msondo Ngoma Music Band, na Mlimani Park Orchestrta, historia yake inaonyesha kuwa alitoka Kigoma alikozaliwa kwenda Arusha kwa masuala ya soka, ingawa pia alikuwa anajua muziki, akitega kote kote.

Alikuwa winga hatari, hivyo alipata timu mjini Arusha, lakini wakati huo huo akiendelea na kipaji chake cha muziki, ndipo alipoonekana na kujiunga na bendi ya National ya huko. Ni bendi ambayo ilimfanya NUTA Jazz 'Msondo Ngoma' kumnyakua na safari ya ustaa ikaanzia hapo. Hadi leo ni mwanachama na shabiki wa klabu ya Simba.

**Kwa maoni piga 0716 350534**



Hassan Bichuka

## HABARI KIMATAIFA

# Netanyahu aonyesha jeuri, asisitiza kuivamia Rafah

**TEL AVIV,** ISRAEL

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amesema nchi yake inaweza kujitegemea baada ya Marekani kutishia kusitisha usambazaji wa silaha ikiwa jeshi litafanya uvamizi kamili katika mji wa Rafah.

Netanyahu amekuwa katika shinikizo kali kutoka Marekani kuacha mpango wake wa kuuvamia kijeshi mji huo ulioko kusini mwa Ukanda wa Gaza.

"Tukihitaji tutajitegemea. Nimesema ikibidi tutapigana kwa jino na ukucha," alisema Netanyahu.

Rais wa Marekani, Joe Biden alisema atazuia baadhi ya silaha ikiwa ni pamoja na mizinga ikiwa mji wa Rafah utavamiwa.

Marekani tayari imesitisha shehena ya mabomu kutokana na hofu ya kusababisha vifo vya raia.

Akizungumza juzi, Netanyahu alikariri vita vya mwaka 1948 na kutupilia mbali onyo kutoka Marekani ambaye ni mshirika wa karibu wa Israel.



"Katika Vita vya Uhuru miaka 76 iliyopita, tulikuwa wachache dhidi ya wengi, hatukuwa na silaha. Kulikuwa na vikwazo vya silaha kwa Israel, lakini kwa nguvu kubwa ya kiroho, ushujaa na umoja kati yetu sisi tulikuwa washindi." alisema

Alisisitiza kuwa Israel ina zaidi ya kucha zao na ikiwa Rais Biden atasitisha usambazaji wa silaha,kwa nguvu hiyo ya kiroho, na kwa msaada wa Mungu, watashinda.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Israel, Yoav Gallant, alisema maadui wa Israel pamoja na marafiki wao bora wanapaswa kuelewa kwamba nchi yao haiwezi kutawaliwa.

"Tutasimama imara, tutafikia malengo yetu." Alisema Gallant.

Maoni hayo yanawadia saa chache baada ya Umoja wa Mataifa, kueleza zaidi ya watu 80,000 wamekimbia mji wa Rafah tangu Jumatatu huku kukiwa na mashambulizi ya mara kwa mara ya anga na vifaru vikiendelea kukusanyika karibu na maeneo ya makazi.

Umoja wa Mataifa pia ulionya kwamba chakula na mafuta yanaelekea kwisha na watu zaidi ya milioni moja bado wamejificha ndani ya jiji hilo.

Wakati huo huo, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, linatarajiwa kulipigia kura azimio litakalotoa haki na hadhi mpya kwa Palestina.

Pia azimio hilo linataka Baraza la Usalama, kuangalia upya ombi la Palestina kuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa.

Mnamo Aprili 18, Marekani ilipinga azimio lililopata uungwaji mkono kutoka nchi mbalimbali ambalo lingetoa mwanya kwa Palestina kutambuliwa kama mwanachama kamili wa Umoja wa Mataifa, kitu ambacho Wapalestina wanapigania kwa muda mrefu.

Naibu Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa Robert Wood, alisema kwamba nchi yake inapinga azimio hilo la Baraza Kuu, akiongeza kuwa njia pekee ya kupata uanachama kamili wa Palestina ni kupitia mazungumzo na Israel.

Uhispania, Ireland na nchi nyingine wanachama wa Umoja wa Ulaya, zinapanga kulitambua taifa la Palestina Mei 21, kulingana na mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya Josep Borrell.

**BBC**




Wafuasi wa Chama cha ANC, Afrika Kusini wakiwa katika harakati za kampeni za uchaguzi utakaofanyika Mei 29 mwaka huu. **PICHA: GATTY IMAGES**.

# Mazungumzo ya amani Sudani Kusini yaanza

**NAIROBI,** AFRIKA KUSINI

MAZUNGUMZO ya kuleta utulivu nchini Sudani Kusini yameanza, huku wito ukitolewa na marais wa nchi za Kiafrika kumalizwa kwa mzozo ambao umedumaza uchumi wa taifa hilo.

Mkutano wa mazungumzo hayo ulifunguliwa jana jijini Naorobi nchini Kenya.

Katika mkutano huo, Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir pamoja na kumshukuru mpatanishi mkuu Rais wa Kenya, William Ruto, ameahidi serikali yake itafanya mazungumzo hayo kwa nia njema na kwa uwazi.

"Makundi ya upinzani yana nia sawa na hamu ya amani nchini Sudan Kusini ambayo baada ya kupatikana kikamilifu, italeta utulivu wa wakati wote na maendeleo ya kiuchumi katika eneo hilo" alisema Kiir.

**Mkutano wa mazungumzo hayo ulifunguliwa jana jijini Naorobi nchini Kenya.**

Kiongozi wa kundi la Real SPLM, Pagan Amum Okiech, alisema wanahitaji kuacha mawazo ya migogoro, kujiona maadui kwa sababu wote ni ndugu.

"Rais Kiir, sisi ni ndugu na jamaa," alisema Okiech.

Mazungumzo hayo yanavikutanisha vikundi vya waasi na serikali kujadili namna ya kumaliza mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yaliyodumu kwa miaka mingi.

Marais wa nchi mbalimbali za kiafrika walihudhuria mkutano huo akiwamo Lazarus Chakwera (Malawi), Hakainde Hichilema (Zambia), Nangolo Mbumba wa Namibia na Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kati, Faustin Archange Touadera.

**DW**

# Jenerali Deby mshindi nafasi ya urais Chad

**N'DJAMENA,** CHAD

KIONGOZI wa kijeshi wa Chad, Mahamat Deby ametangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi wa urais na kuendelea kuongoza nchi hiyo kwa kipindi kingine.

Baraza la Uchaguzi la nchi hiyo lilimtangaza Jenerali Deby mshindi kwa kupata asilimia 61.3 ya kura, akimbwaga mpinzani wake Waziri Mkuu Succes Masra, ambaye alipata asilimia 18.53 za kura zote.

Masra alitangaza kwamba yeye ndiye mshindi katika duru ya kwanza ya upigaji kura, na kwamba ushindi aliopata Deby ulitokana na wizi wa kura.

Jenerali Deby (40), alitawazwa kama kiongozi wa Chad na jeshi baada ya baba yake, Idriss Deby Itno, kuuawa wakati wa vita na vikosi vya waasi Aprili, 2021.

Matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika Jumatatu, yalitangazwa wiki mbili mapema kuliko ilivyotarajiwa.

Kabla kutangazwa matokeo hayo, mgombea wa upinzani Waziri Mkuu Masra alidai kushinda kwa kupita matangazo ya moja kwa moja kwenye mtandao wa Facebook, na kutoa wito kwa wafuasi wake na vikosi vya usalama kupinga kile alichosema ni jaribio la Jenerali Deby kuiba ushindi kutoka kwa watu wa Chad.

Chad inakuwa nchi ya kwanza kati ya nchi ambazo jeshi lilinyakua mamlaka katika Afrika Magharibi na Kati katika miaka ya hivi karibuni kufanya uchaguzi na kurejesha utawala wa kiraia. **BBC**



# Kambi ya siku tisa, watu 300 wakutwa na kisukari

**Na Halfani Chusi**

KATI ya wagonjwa 1,050 waliopimwa kupitia kambi ya matibabu bure iliyofanyika katika Hospitali ya Istiqama, Magomeni, mkoani Dar es Salaam, watu 300 wamekutwa na matatizo ya kisukari na presha.

Kambi hiyo ya siku tisa iliyomalizika jana, ilifanywa na jopo la madaktari bingwa sita kutoka Ujerumani kwa kushirikiana na wa kutoka hospitalini hapo.

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Abdalah Mohamed, aliyasema hayo katika hafla ya kuwaaga madaktari hao, hafla iliyohudhuriwa pia, na viongozi kutoka Wizara ya Afya.

Alisema katika operesheni hiyo, wamefanikiwa kuwafanyia upasuaji wagonjwa 45 na tayari wameruhusiwa, huku wengine 25 wakiendelea na matibabu chini ya uangalizi wa hospitali hiyo.

"Katika kambi hii, tumewafikia wagonjwa mbalimbali wa presha na kisukari wapatao 300, wenye matatizo ya mifupa 200, masikio, pua na koo 150, figo 100. Madaktari hawa pia, wamebaini kuna wagonjwa wengi wa saratani, lakini kwa bahati mbaya wataalamu wake hawakuwapo, tunatarajia kambi ijayo watakuja," alisema.

Mohamed alisema katika utafiti uliofanywa na madaktari hao, wamebaini watanzania wengi wana matatizo ya afya, lakini kutokana na huduma za matibabu kuwa juu wanashindwa na hivyo, kupeleka wengi kupoteza maisha.

Alizitaja huduma nyingine zilizotolewa katika kambi hiyo ni za upasuaji wa nyama ya pua, na uvimbe ndani ya tumbo na nje.

Mratibu wa Tiba Utalii na Mratibu wa Tiba Nje ya Nchi, Dk. Asha Mahita, akizungumza kwa niaba ya Wizara ya Afya, aliushukuru uongozi wa hospitali kwa kuratibu kambi hiyo na kusaidia kuwapatia matibabu watanzania 1,050.

"Tunawashukuru sana kwa kushirikiana, ninaomba mwendelee hivihivi isiwe tu Dar es Salaam, ikiwezekana tuzunguke nchi nzima. Huduma za afya ni gharama kwa bahati mbaya wengi hatujui thamani ya afya, ifike mahali tuzingatie ushauri wa wataalamu ili kuepukana na maradhi yanayoweza kuzuilika," alisema.

Aidha, alisema anatamani mbali na matibabu hayo, elimu itolewe kuhusu mfumo wa maisha na vyakula, akisistiza Istiqama ni taasisi ya muda mrefu, ina vitu vingi vya kusaidia wananchi.

Mkurugenzi wa Elimu Bridge Words, Dk. Fahdy Hemed, alisema lengo la kambi hiyo lilikuwa kuwasaidia wagonjwa wasio na uwezo wa kifedha kupata matibabu ya kibingwa.

"Hatukutegemea watu wengi, wagonjwa wamefika kwa wingi, safari ijayo tutajipanga zaidi kufanya mambo makubwa. Tumefanya hivi pia kuiunga mkono serikali," alisema.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kushoto) akijadiliana jambo na Mbunge wa jimbo la Handeni Mjini, Reuben Kwagilwa, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CHADEMA wajifungia kujadili mambo mazito

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), inatarajia kufanya kikao chake kwa zaidi ya siku tatu mfululizo kuanzia leo, huku ikidaiwa miongoni mwa hoja zitakazojadiliwa ni pamoja na kauli ya Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu, kuhusu fedha chafu ndani ya chama.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA , John Mrema, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana alisema pamoja na mambo mengine, kamati hiyo itajifungia kujadili hoja kuu tatu.

Alitaja miongoni mwa hoja hizo ni pamoja na kupokea taarifa ya chaguzi katika ngazi mbalimbali za chama, kupokea taarifa ya tathmini ya maandamano ya awamu ya kwanza ya mikoa katika wiki ya maandamano na kuweka mwelekeo wa awamu ya pili ya maandamano hayo.

Hoja nyingine alisema ni kufanya usaili na kuteua wagombea nafasi za uongozi katika kanda nne za Nyasa, Serengeti, Victoria na Magharibi.

Kikao hicho kimeitishwa kukiwa bado na mjadala unaoendelea kwenye mitandao ya kijamii na katika ‚vijiwe' mbalimbali juu ya kauli zilizotolewa hivi karibuni na Lissu na miongoni ni madai ya uwapo wa fedha chafu katika chaguzi za ndani za chama hicho zinazoendelea.

Tangu Lissu atoe kauli za kudai kwamba ndani ya chama hicho kuna fedha chafu, hakuna kauli nyingine iliyotolewa na viongozi wengine wakuu wa CHADEMA.

Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, alipoulizwa msimamo wa chama kuhusu jambo hilo, hakuwa tayari kusema lolote, japokuwa katika moja ya magazeti nchini alinukuliwa akisema, jambo hilo pamoja na mengine yatajadiliwa kwenye vikao vya chama.

Moja ya mjadala kwenye mitandao ya kijamii, baada ya kutoka kwa taarifa ya kikao hicho cha Kamati Kuu, ni matarajio ya kujitokeza kwa mjadala wa madai ya kuwapo wa fedha hizo chafu kwenye chaguzi za ndani zinazoendelea.

Akiwa kwenye mkutano wa hadhara Mpwapwa mkoani Dodoma, Mei 8, mwaka huu, Lissu alisema anashangaa kushambuliwa na watu baada ya kauli yake hiyo na wengine wakisema, hakuwa na haja ya kusema hadharani, bali kwenye vikao ndani ya chama chake.

"Nimeshangaa sana watu wanishambulia kwa sababu ya kauli yangu niliyoitoa Iringa Mei 2, mwaka huu, kwamba ndani ya chama chetu kuna fedha chafu, eti wanasema kwa nini nisingeisemea ndani kwenye vikao. "Rushwa si ya kunyamazia, tutaikemea ndani ya CHADEMA na tutaikemea nje ya CHADEMA, na tutaikemea hadharani halafu baada ya hapo ndio tunakwenda kwenye vikao," alisema Lissu.

Uchaguzi unaoendelea ndani ya chama hicho ni pamoja na wa ngazi ya kanda ambao Kanda ya Nyasa ndiyo ina ushindani mkubwa kulinganisha na zingine. Mbunge wa zamani wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi (Sugu) na Peter Msigwa anayetetea nafasi hiyo ambaye pia ni mbunge wa zamani wa Iringa Mjini ndio wanaochuana.

## Mwinyi aahidi kuchangia uendeshaji msikiti

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameahidi kuchangia nguvu za uendeshaji wa Masjid Quba ili kuongeza ari na hamasa kwa viongozi na waumini wanaoutumia msikiti huo.

Dk. Mwinyi pia amesifu uongozi wa msikiti huo kwa weledi wao wa kutoa taaluma bure kwa vijana na waumini wa dini ya kiislamu na kuwaahidi kuwaongezea nguvu za mahitaji ya msikiti huo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, Dk. Mwinyi alitoa ahadi hiyo jana baada ya ibada ya sala ya Ijumaa katika msikiti huo, Mbweni mkoa wa Mjini Magharibi.

"Maadam na mimi mmenieleza haya mnayoyafanya basi na mimi nitakuchangieni ili tuzidi kuliendesha gurudumu hili," aliahidi.

Akizungumzia suala la kuwaombea dua viongozi wa serikali, Alhaj Dk. Mwinyi aliwasihi waumini na viongozi wa msikiti huo wasichoke kuwaombea dua viongozi wa nchi ili Mwenyezi Mungu azidi kuwapa wepesi wa kutekeleza na kuzikamilisha ahadi walizoziahidi kwa wananchi.

Alhaj Dk. Mwinyi alisema ahadi nyingi tayari zimetekelezwa na kukamilishwa kwa wakati lakini bado zipo nyingi pia zinahitaji kukamilishwa kwa mafanikio makubwa na kueleza maombi mema kutoka kwa wananchi kwenda kwa viongozi wao, bado yanahitajika katika kufikia malengo ya nchi iliyojiwekea na kufanyakazi kwa uadilifu.

Awali, akizungumza kwenye ibada hiyo ya sala ya Ijumaa msikitini hapo, Katibu Mtendaji kutoka Ofisi ya Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisifu juhudi za Alhaj Dk. Mwinyi kwa weledi wake wa kushirikiana na wananchi na waumini wa dini ya Kiislamu kwenye ibada ya sala ya Ijumaa kwa maeneo mbalimbali nchini kutokana na dhamira na nia yake njema kwa watu wa Zanzibar. Alisema uongozi wa Alhaj Dk. Mwinyi ni juhudi zake za kuwafikia wa watu wote pamoja na hudumia kwani ni kiongozi wa wote.

Akitoa hutba kabla ya sala ya Ijumaa, Khatib wa sala hiyo, Sheikh Ali Masoud, amewasihi waumini wa dini ya Kiislam kuwaombea mema na kuwatii viongozi wa nchi, kwani kufanya hivyo ni kulitakia heri na baraka taifa na watu wake.

Baada ya ibada ya Sala hiyo ya Ijumaa, Dk. Mwinyi aliwatembelea wazee, akiwamo Mbunge wa zamani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), jimbo la Amani, Mzee Hassan Rajab, nyumbani kwake, Kisauni wilaya ya Magharibi B" na Mjumbe wa Baraza la Wazee kupitia Chama Cha CCM Kisiwandui, Maryam Hengwa, nyumbani kwake, Kwa Mchina, mkoa wa Mjini Magharibi.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-12

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Mashushushu huonekana kama wachawi hivi kwani anaweza kuepuka jambo baya lililotarajiwa kumpata. Waswahili wanasema machale. Lakini mara nyingi wao hutumia mlango wa sita wa fahamu.

Kwa kawaida binadamu huwa ana hisia tano yaani kuona, kuonja, kusikia,kunusa, kuhisi kwa kutumia ngozi.

Watu wa itelejensia, mashushushu au wapelelezi hutumia hisia ya sita. Ni ipi?

Wataalam wanasema hisia ya sita wanakuwa nayo binadamu wa kawaida tu wenye hisia tano, lakini wao wanafundishwa, kujifunza au kufundwa namna ya kutumia akili waliyonayo kujiongeza, kuwa na uwezo hali ya juu ya kutambua, kuona, au kuhisi jambo ambalo si la kawaida ambalo kwa mtu wa kawaida hawezi kufanya hivyo. Inasemekana wapo waliozaliwa kuwa na uwezo huo wa kuwa na machale, lakini pia unaweza kujifunza. Kamal alikuwa mtu wa aina hiyo.

Alishawahi kuepuka balaa moja lililoelekea kumpata, alipoitwa na demu mmoja kule Bonyokwa.

Kama angekuwa mtu asiye na hisia ya sita, angeweza kupata fumanizi feki, kupigwa, kuibiwa, kujeruhiwa au kuuawa. Ilikuwaje?

Alimpata demu kupitia mitandao ya kijamii kabla ya kumpata Mariamu. Kama kawaida ya baadhi ya vijana ambao huopoa wanawake kwa kutumia mitandao hiyo. Mapenzi yao yakawa motomoto, lakini kupitia simu zao na mitandao.

Demu akamuomba aende nyumbani wake maeneo ya Kongowe, Dar es Salaam. Wakapigiana simu na kukubaliana Jumamosi moja amtembelee. Siku ya tukio, saa 12:00 jioni, Kamal alitoka nyumbani kwake kuelekea kwa mpenzi wake aliyejitaja kwa jina la Paulina.

Alipanda basi la kwenda Mbagala Rangi Tatu na alipofika, ilibidi achukue basi lingine linaloelekea Kongowe hadi Tuangoma.

Wakati huo wote, Paulina alikuwa akimpigia simu kumuuliza amefika wapi. Kama kawaida yake, Jamaa anaishi kiitelejensia sana. Kanuni ni ile ile.

Unapotaka kwenda sehemu yoyote, iwe ya mualiko au kukutana na mtu kwa sababu za kikazi, au zinazofanana na hizo, au hata wewe mwenyewe umewaita kukutana nao, na una mashaka, basi usalama wako ni kuchelewa kwenye ahadi au kuwahi.




**“Saa hizi yupo njiani, amepanda basi ya kuja huku, akija tu akishuka nitamkumbatia, mtapiga picha ya video. Nitampeleka pale kwenye kioski cha Mpemba kunywa juisi, pale nyinyi mtatokea, mmoja akijifanya mume wangu, tutafanya fumanizi feki, mimi nitajifanya nalia na kuomba msamaha, kama kawaida, mtamkomba kila kitu. Mimi nitatoka hapo najifanya kukimbia, halafu nyinyi mtajua la kumfanya, tutakutana mbele.”**

Ukiwahi unakuwa umejiwekea mazingira mazuri ya kumsoma au kuwasoma uliowaita, waliokuita au kukualika, na jitahidi wewe uwaone kabla wao hawajakuona, unaweza kujua nia yao ni nini. Kwa sababu wanaweza kufanya kitu ambacho ukahisi siyo watu wazuri kwako na wanakuita kwa ajili ya kukudhuru.

Kuchelewa pia kuna manufaa, kwani wanaokusaka kwa mabaya wanakuwa hawako kwenye hali ya kawaida, wameshaanza kuhamanika na kuulizana. Hili unaweza kulitambua pale utakapofika na kuanza kuwaona kabla wao hawajakuona.

Wakati anapanda basi kwenda Kongowe akampigia Paulina kuwa bado kitu kimoja afike Mbagala Rangi Tatu. Lengo ni kumfanya kufahamu kuwa mgeni wake bado yupo mbali.

Alipofika Kongowe, akateremka na kuzima simu yake. Sababu ili kuwa ni kutaka kumuwinda na kumuona mtu aliyeahidiana naye kabla hawajakutana. Alifahamu fika ni mmoja kati ya watu waliokuwa pale kwenye kituo cha kuteremkia, au pembeni yake akimsubiri mgeni wake, hivyo kitendo cha kuicha simu yake wazi, anayemsubiri anaweza kupiga ili kufahamu yupo wapi, halafu ikaanza kuita, kumbe wote wapo karibu.

Akavuka barabara na kwenda ng'ambo ya pili. Akaenda kusimama pembeni kidogo ya kibanda cha wakala wa simu. Akawasha simu na haraka akaipiga. huku macho yake yakiangalia kule alikoteremkia.

Akatabasamu. Kwa macho yake, akamshuhudia msichana mmoja, akiweka simu yake sikioni. Alichomwambia ni kwamba ameshapanda basi la kwenda Kongowe. Tayari alikuwa amekamilisha kazi ya kwanza. Ni kumfahamu mwenyeji wake. Kazi ya pili ilikuwa ni kufahamu kama ni mwenyeji salama au la? Kumbuka Kamal anaishi kwenye njia zile zile za ushushushu, kazi ambayo aliipenda sana, lakini hakufanikiwa kuipata kwa ajili ya kuitumikia nchi. Kilichobaki alikuwa akitumia mbinu hizo yeye mwenyewe kwa ajili ya usalama wake au watu wake wa karibu, wakati mwingine kujifurahisha kwani ni mpenzi sana wa michezo hiyo. Vitabu vya kipelelezi na filamu za kishushusu, zilimfundisha mambo mengi anayoyahusudu.

Alichofanya sasa ni kuvuka barabara na kumfuata mwenyeji wake. Lengo ni kumuagalia kwa karibu, pamoja na kufuatilia nini anafanya kabla ya yeye kufika. Alijua atafanya kwa uhuru mkubwa kwa sababu hatojulikana. Alichokiona, pamoja na kumtisha, lakini ndicho kilichofanya afurahie kuishi kishushushu.

Kwa macho yake alishuhudia yule dada akiwaita wanaume wawili na kuwataka wakajifiche mahali kabla yeye hajafika.

“Saa hizi yupo njiani, amepanda basi ya kuja huku, akija tu akishuka nitamkumbatia, mtapiga picha ya video. Nitampeleka pale kwenye kioski cha Mpemba kunywa juisi, pale nyinyi mtatokea, mmoja akijifanya mume wangu, tutafanya fumanizi feki, mimi nitajifanya nalia na kuomba msamaha, kama kawaida, mtamkomba kila kitu. Mimi nitatoka hapo najifanya kukimbia, halafu nyinyi mtajua la kumfanya, tutakutana mbele.”

Meneno hayo ya Paulina yalisikika vizuri tu masikioni mwa Kamal. Yalikuwa ni ya hatari lakini yalimfanya afurahi na kuangua kicheko cha chini chini. Akajipongeza mwenyewe kwa kuwa mtu wa tahadhari kwa kila kitu kama shushushu wa kimataifa. Kumbe kule kuitwa kote na mwanamke aliyefahamiana naye mtandaoni alikuwa ni kama mbuzi anayepelekwa machinjioni. Alijipongeza kwa kuwa mtu wa machale. Angekuwa mtu wa kawaida, yangempata makubwa.

Alichofanya ni kupanda basi lingine, na kurejea Mbagala, kabla ya kurudi nyumbani kwake. Alipopigiwa na Paulina amefika wapi akamwambia amerejea nyumbani kwake kwa sababu amepigiwa simu ya dharula, hivyo wangeonana wakati mwingine. Mshtuko, lawama, maneno na matusi, aliyoyapata kutoka kwa mwanamke huyo, yalithibitisha kuwa hakuwa mtu nzuri.

Alifika mapema mno. Saa nzima kabla ya Teddy kufika. Lengo ni lile lile. Pamoja na kumuamini Teddy, lakini kanuni moja ya ushushushu inasema usimumini mtu yoyote, hata kama ni baba au mama yako mzazi. Hiyo tu ilitosha kumuelekeza kuwa hata Teddy asiaminike. Hata kama si yeye kutumwa, lakini anaweza kuwa kuna watu wanafutilia nyuma, hasa baada ya kutoka nyumbani kwake kuchukua vitu vyake na kumletea pale alipo.

“Umeshafika?” Kamal alimuuliza kwa njia ya kumpigia simu. “Bado ila niko njiani karibuni nifike, wewe je?” “Mimi ndiyo bado kabisa.” “Basi mimi nitakusubiri.” “Sasa unasikia Teddy, ukifika kaa pale kwenye benchi la kituo cha mwendokasi hapo, mimi nitakuta hapo hapo.” “Sawa shemeji.” Akaitikia Teddy.

*Itaendelea Jumamosi*

HABARI MICHEZO

# NAHODHA SIMBA AFURAHISHWA NAMNA WALIVYOPAMBANA KUIFUNGA AZAM FC

**Na Faustine Feliciane**

NAHODHA wa Simba, Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr' amesema amefurahishwa na namna walivyopambana kuhakikisha wanapata alama tatu mbele ya Azam FC.

Zimbwe alisema ushindi walioupata juzi umetokana na wachezaji kujituma muda wote wa mchezo na kufuata maelekezo ya makocha wao.

„Ni ushindi muhimu sana kwetu, kila mmoja alijitoa kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, tunashukuru tumefanikisha hilo na sasa tunaangalia michezo iliyobakia mbele yetu," alisema Zimbwe.

Simba juzi ilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Azam katika mchezo uliochezwa uwanja wa Benmjamin Mkapa jijini dar es Salaam.

Magoli ya Simba katika mchezo huo yalifungwa na Sadio Kanoute, Fabrice Ngoma na David kameta ‚Duchu'.

Zimbwe alisema licha ushindi huo, mchezo ulikuwa mgumu kutokana na ubora wa wapinzani wao ambao nao walikuwa na kiu ya kupata ushindi.

„Tuliwafunga kwenye mchezo wa fainali Ligi ya Muungano kule Zanzibar,. hivyo tulitegemea mchezo huu ungekuwa mgumu kwa sababu wasingekubalui kirahisi kupoteza tena, walipambana lakini nadhani sisi tulikuwa bora zaidi," alisema Zimbwe.

Matokeo hayo ya juzi yameifanya Simba kufikisha pointi 56, pointi moja nyuma ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili lakini wekundu haowakiwa na faida ya kuwa na mchezo mmoja mkononi.

KIKAPU




Wachezaji wa mpira wa Kikapu kwa Walemavu wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam kama walivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Pointi 3 tu Simba Queens bingwa

**Na Saada Akida**

Simba Queens inahitaji pointi tatu tu kwenye michezo mitatu iliyobaki ya Ligi kuu ya wanawake kuweza kutangaza ubingwa msimu wa 2023/2024.

Mpaka sasa SImba Queens inaongoza msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 43 wakiwazidi kwa alama tisa JKT Queens inayoshika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Simba Queens wamebakiza mechi dhidi ya Alliance Girls watakaocheza ugenini Mei 29 kabla ya Juni 3 kuumana na Fountain Gate Princess nyumbani na baadae kucheza mchezo wa mwisho Juni 7 dhidi ya Geita Gold Queens kwenye uwanja wa Azam Complec jijini Dar es Salaam.

Wekundu hao wa Msimbazi kama watafanikiwa kushinda michezo yote mitatu watafikisha pointi 52 wakati wapinzani wao wa karibu, JKT Queens kama watashinda mechi zao tatu zilizobakia watafikisha pointi 43.

Msimu huu Simba imedhamiria kurejesha heshima yao kwa kuhakikisha wanafanikiwa kutwaa ubigwa baada ya msimu uliopita kuupoteza mbele ya JKT Queens.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan ‚Mgosi', alisema malengo yao ni kuona wanatwaa taji hilo bila ya kupoteza mechi.

Alisema katika soka sio rahisi lakini wanaweza kufikia malengo hayo kama wachezaji wake wataendeleza umakini na kasi waliyonayo ambayo imekuwa chachu ya matokeo mazuri msimu huu.

"Hatuangalii mechi, tunahitaji kushinda kila mechi bila ya kujali tunakutana na timu ipi, hatupaswi kubweteka kwa matokeo na nafasi tuliyo sasa, wachezaji wanatakiwa kutambua ligi haijaisha na kama tutapoteza umakini tunaweza kupoteza malengo, " alisema Mgosi.

## Kocha alalamikia viwanja Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa timu ya Mafunzo SC, Shekha Khamis, amevilalamikia Viwanja vya Mau vinavyotumika kwenye michezo ya Ligi Kuu Zanzibar kuwa vinachangia kuumia kwa wachezaji kutokana na ubovu wake eneo la kuchezea

Akizungumza na Waandishi wa habari jana, alisema nyasi bandia zilizopo katika uwanja huo zimechoka na kuchanika na ardhi ngumu ya chini ya nyasi hizo kuja juu na kusababisha majeraha ya mara kwa mara kwa wachezaji.

„Kulingana na hali ya uwanja huu, majeruhi hawakauki kwa timu mbalimbali ikiwemo timu yangu, nadhani wahusika wanapaswa kulitazama hili na kulifanyia kazi," alisema Khamis.

Alisema hivi sasa katika kikosi chake kuna wachezaji wengi ambao ni majeruhi na wengi wanalalamika maumivu ya miguu pamoja na nyama za paja nan sababu kubwa ya kuumia ni mindombinu ya uwanja.

Alisema Bodi ya Ligi Zanzibar iangalie tena hali ya Uwanja huo kwa hivi sasa katika kipindi hiki ambacho ligi imekuwa katika kasi kubwa.

"Kila baada ya mechi tunawatibu wachezaji wetu, wanaumwa na maumivu makali ya mwili, tunacheza mpira katika uwanja ambao ni hatari mtu akianguka vibaya basi anaweza kupata majeraha mabaya sana"alisema kocha huyo.

Aidha Akizungumza na gazeti Nipashe, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Issa Kassim, alisema Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) linaangalia uwezekano wa kuhamisha michezo inayochezwa kwenye uwanja huo.

## New City FC na matumaini kubaki Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA msaidizi wa New City FC, Razak Salum Rajab 'Wenger' amesema bado wana matumaini makubwa ya kubaki Ligi Kuu ya Zanzibatr licha ya matokeo mabaya waliyoyapata hivi karibuni.

Kauri hiyo ya Rajabu imekuja siku moja baada ya kikosi chake kuibuka na ushindi wa bao 2-0 dhidi ya Kipanga FC.

Kwa matokeo hayo ya juzi, New City FC imepanda kwa nafasi mbili juu kutoka nafasi ya 12 mpaka nafasi ya 10 baada ya kufikisha pointi 27.

Akizungumza mjini hapa, Kocha huyo alisema bado ndoto na malengo yao ni kuhakikisha wanafanikiwa kuinusuru timu hiyo kutoshuka daraja.

Alisema katika michezo mitatu waliyocheza wamefanikiwa kuvuna alama tano alama ambazo zinaendelea kumpa matumaini makubwa ya kubaki Ligi kuu.

Aidha, alisema kikubwa wanachofanya hivi sasa ni kuwaongezea hamasa wachezaji wao na kusahahu matokeo ya michezo ya nyuma ambayo hawakufanya vizuri.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUMPIGA BEI JESUS
ARSENAL ipo tayari kusikiliza ofa za kumuuza mshambuliaji wao raia wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miak 27 msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### WATAKIWA SAUDI ARABIA
KIUNGO wa kati wa Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 30, na Gabriel Jesus wanasemekana kuwa kwenye rada za klabu kadhaa nchini Saudi Arabia. ***(Express)***

### CALLUM WILSON HAKIELEWEKI
MUSTAKABALI wa mshambuliaji wa Newcastle United, Callum Wilson bado haujulikani huku Mwingereza huyo mwenye umri wa miaka 32 akihusishwa na uwezekano wa kuondoka pale St James' Park. ***(Mirror)***

### TUCHEL NA MAN UNITED
KOCHA anayeondoka wa Bayern Munich, Thomas Tuchel ndiye anayeongoza kuwania nafasi ya kocha ajaye wa Manchester United huku klabu hiyo ya Ligi ya Kuu England iikilenga kuiziba nafasi ya Erik ten Hag. ***(Football Insider)***

### SANCHO KUBAKI DORTMUND
KLABU ya Borussia Dortmund inataka kusalia na winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo msimu ujao kwa sababu uhamisho wa kudumu kutoka Manchester United kwa sasa hauwezekani na gharama yake ni ya juu kwa klabu hiyo ya Ujerumani. (***Sky Sport Ujerumani***)

### MAN FEDHA KIBAO
KLABU ya Manchester United inatumaini kupata pauni milioni 100 kwa kumuuza mshambuliaji Jadon Sancho na Muingereza Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22, msimu huu wa majira ya joto. ***(Give Me Sport)***


### GUIRASSY ATAKIWA ARSENAL
MSHAMBULIAJI wa Stuttgart kutoka Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 28, ameonekana kutakiwa na Arsenal huku Mikel Arteta akijaribu kuimarisha safu yake ya ushambuliaji. ***(Fichajes)***

### KELVIN PHILLIPS NA LEEDS
MATUMAINI ya kiungo wa kati wa England, Kelvin Phillips kuungana tena na Leeds United msimu huu wa joto yanategemea timu hiyo ya Elland Road kupata nafasi ya kurejea Ligi Kuu. ***(Football Insider)***

### MARIO HERMOSA AWINDWA
KLABU ya Aston Villa inakaribia kumsajili beki wa Atletico Madrid, Mario Hermoso mwenye umri wa miaka 28. ***(AS)***

### DAVID ATAKIWA MILAN
KLABU ya AC Milan ipo tayari kufikiria kumsajili mshambuliaji wa Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24 kutoka Lille katika dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto ***(Calciomerca)***

## DON ZA SOKA MAGA YA ULAYA




# KIUNGO JORGINHO ASAINI MKATABA MPYA ARSENAL

## Nyota huyo wa zamani wa Chelsea sasa kubaki kwa ‚washika bunduki' hao mpaka...

**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Jorginho ameongeza mkataba mpya utakaomweka klabuni hapo hadi msimu wa joto wa 2025.

Jorginho aliwasili kutoka kwa wapinzani wao wa London, Chelsea Januari 2023 na amekuwa mchezaji muhimu wa kocha Mikel Arteta kwenye kikosi chake, akicheza mara kwa mara.

"Tunafuraha kwamba Jorgi ametia saini mkataba mpya nasi," Arteta aliiambia Arsenal.com.

"Jorgi ni sehemu muhimu ya timu yetu, mfano wa kuigwa na ujuzi mkubwa wa uongozi na uwezo wa kipekee wa kucheza ambao unafanya kila mtu kuwa bora zaidi karibu naye uwanjani.

Tunafurahi sana kwamba Jorgi na familia yake wamejitolea na sisi. wote tunafurahi kuendelea na safari hii pamoja."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 32 alisema muda wake Arsenal umekuwa „chanya" hadi sasa, akisisitiza haukuwa uamuzi mgumu kujitolea tena.

"Nilihisi sehemu ya kitu kikubwa mara moja. Nilihisi kuhusika na kwa kweli mahali pazuri. Sio hivyo kila wakati, kwa hivyo unapohisi kitu kama hiki, ni kitu muhimu," alisema.

"Nimefurahi sana kubaki, kwa sababu ni bahati kuwa sehemu ya familia hii. Familia yangu ina furaha, tumekaa vizuri na kuna mengi yanakuja! Hakukuwa na mengi ya kujadili kuwa mkweli kwa sababu nahisi kweli, vizuri kuwa hapa. Kujua tu kwamba wananithamini na kunitaka nikae kwa muda mrefu vilevile, ni jambo kubwa kwangu ninahisi kwamba nina mengi ya kufanya, kwa hiyo ndiyo sababu ninakaa," alisema Jorginho

HABARI MICHEZO

# Pickford asakwa Stamford Bridge

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imeendelea kufanya mazungumzo na golikipa wa Everton, Jordan Pickford, ili kumshawishi ajiunge nao dirisha lijalo la majira ya kiangazi kwa ajili ya kuboresha eneo lao la ulinzi.


Pickford mwenye umri wa miaka 30 ni mmoja kati ya makipa wilioonesha kiwango bora msimu huu na hadi sasa anashika nafasi ya pili kwa kucheza mechi nyingi bila ya kuruhusu bao akiwa amefanya hivyo katika mechi 12 za EPL, nyuma ya David Raya.

Kipa huyo amekuwa tegemeo katika kikosi cha timu ya taifa ya England na klabu yake msimu huu ambapo amecheza mechi 40 za michuano yote.

Licha ya uwepo wa Djordje Petrovic na Robert Sanchez, benchi la ufundi la Chelsea limeonyesha kutoridhishwa na viwango vyao, hivyo wanahitaji kufanya maboresho zaidi.

Mkataba wa Pickford unamalizika mwaka 2027 na Everton huenda ikahitaji zaidi ya Pauni 50 milioni kwa ajili ya kumuuza.





# ARTERA AWATAKA JESUS, MARTINEL 'KUZUNGUMZA' ZAIDI UWANJANI

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amewataka washambuliaji wake, Gabriel Jesus na Gabriel Martinelli ‚kuzungumza' zaidi uwanjani ili kumshawishi kuwapa nafasi kwenye kikosi cha kwanza huku timu hiyo ikiendelea kutafuta taji la Ligi Kuu England msimu huu.

Jesus na Martinelli wamejikuta nje ya kikosi cha kwanza cha Arteta katika wiki za hivi karibuni huku Leandro Trossard, Kai Havertz na Bukayo Saka wakiibuka kama chaguao la kwanza la Muhispania huyo.

Alipoulizwa na ESPN Brasil ikiwa wawili hao walikuwa wamechanganyikiwa na utaratibu uliopo, Arteta alisema: „Nadhani kuna sehemu mbili. Moja, wanafuraha kwa sababu ya mahali tulipo kama timu na kile tunachopigania. Na nyingine kwa sababu sasa wanataka kucheza.

„Kila mtu ambaye hachezi anataka kucheza zaidi. Lakini huo ni uamuzi wangu na kile ninachohisi kila wakati.

„Wote wawili wamekuwa muhimu sana msimu huu, na pia itakuwa michezo miwili iliyosalia na hii ndio inahusu, unapopata nafasi ya kucheza lazima uzungumze kwa vitendo uwanjani," alisema Arteta.

Mustakabali wa Jesus katika klabu hiyo umekuwa shakani huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil akikabiliwa na matatizo ya goti tangu afanyiwe upasuaji wa jeraha alilolipata kwenye Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar.

Alifanyiwa upasuaji mdogo wa pili Januari na alikiri mwezi uliopita kuwa hakumbuki ni lini siku ya mwisho alicheza soka bila maumivu.

Katika mkutano wake na wanahabari Ijumaa iliyopita, Arteta alisema klabu hiyo haina nia ya kumruhusu Jesus kuondoka, na aliiambia ESPN Brasil kwamba jeraha ndio sababu kuu ambayo imemfanya asitumike zaidi msimu huu.

# Dest kurejea Barcelona

**AMSTERDAM, Uholanzi**

PSV Eindhoven itaachana na mpango wake wa kutaka kumpa mkataba wa kudumu Sergiño Dest baada ya beki huyo wa Marekani kuumia mguu kwenye mazoezini mwezi uliopita, vyanzo viliiambia ESPN.

Dest mwenye umri wa miaka 23, amekuwa tegemeo kubwa katika kikosi cha PSV msimu huu waliposhinda Ligi Kuu, huku kocha Peter Bosz hivi majuzi akionesha nia ya kutaka kusalia naye zaidi ya majira ya kiangazi.

Hata hivyo, kwa kuwa Dest sasa anakabiliwa na miezi ya nje ya uwanja, badala yake atarejea rasmi katika klabu yake kuu ya Barcelona kuanzia Julai mosi.

PSV ilimsaini Dest kwa mkopo wa msimu uliopita mwaka jana katika mkataba ambao ulijumuisha chaguo lao kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu msimu huu wa majira ya joto kwa Euro milioni 11.

Dest alicheza mechi 36 kwa mabingwa hao wa Uholanzi katika mashindano yote kabla ya kuumia mazoezini Aprili 20.

Beki huyo wa pembeni alithibitisha wiki iliyopita kwamba alikuwa anahitaji kufanyiwa upasuaji, hivyo basi ataondolewa kwenye kikosi cha Marekani kinachotarajia kushiriki michuano ya Copa America msimu huu wa kiangazi.

Vyanzo vimeongeza kuwa PSV inaweza kumtaja tena Dest atakapokuwa fiti, ingawa hakuna uwezekano wa kumtumia tena katika kipindi kilichosalia.

Mkataba wa Dest na Barca unamalizika 2025, kwa hivyo anaweza kuondoka katika klabu ya Kataluny kama mchezaji huru.



HABARI MICHEZO

# SIMBA KUIBOMA AZAM DIRISHA LA USAJILI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umepanga kupiga hodi kwenye klabu ya Azam kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kumsajili kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Ayoub Lyanga, imefahamika.

Mkataba wa Lyanga na Azam unafikia mwishoni mwa msimu huu na tayari mabosi wa Azam wameanzisha mazungumzo ya kumuongezea mkataba licha ya Simba nao kuweka dau lao mezani kwa nyota huyo.

Taarifa zilizopatikana jana mchana kutoka ndani ya klabu ya Simba, zinasema viongozi wa timu hiyo wanataka huduma ya Lyanga kufuatia maamuzi ya kutaka kuongeza idadi ya mawinga kwenye timu hiyo.

"Ayoub mkataba wake unaisha mwishoni mwa msimu huu, kuna ofa zimefika mezani ikiwemo ya Simba na pia inaelezwa Yanga nao wanamtaka, lakini Azam nao wanataka kubaki naye na wameshaanza mazungumzo ya kuongeza mkataba," alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo.

Aliongeza kwa kuwa timu zote zimeonyesha nia ya kumtaka, mchezaji huyo kwa sasa anaangalia kwenye ofa nzuri ingawa ameipa kipaumbele klabu yake ya sasa ya Azam FC.

Nipashe lilimtafuta Ofisa habari wa Azam FC, Thabit Zakaria 'Zaka', ambaye amethibitisha timu hiyo kuwa kenye mazungumzo na Ayoub kwa ajili ya kumuongezea mkataba licha kuwepo kwa tetesi za kutakiwa na timu nyingine.

„Tuko naye kwenye mazungumzo, suala la kuendelea kutumikia Azam FC au vinginevyo litakuwa jukumu lake, tunamuhitaji badop na ndio maana tumeanzisha mazungumzo kwa ajili ya mkataba mpya," alisema Zaka na kuongezea,

"Nyota huyo yupo kwenye mipango yetu ya msimu ujao , tunafanya jambo la haraka kuzungumza naye ili kuweza kusalia ndani ya kikosi, kama ataona ofa nzuri na kutaka kubadilisha changamoto kwetu hatuna pingamizi, " alisema Ofisa huyo.

SOKA



Vijana wanaolelewa katika Kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi ya mpira wa miguu katika viwanja vya Kituo hicho jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kifaru aanza nyodo Mtibwa kupata ushindi

**Na Adam Fungamwango**

BAADA kutoa kipigo kizito cha mabao 3-0 kwa Tabora United, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru amesema wamefufua matumaini ya kubaki Ligi Kuu huku akitamba watahakikisha wanashinda mechi zote nne walizosalia nazo kabla ya ligi kufikia tamati.

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro, Kifaru amesema wapo watu walioanza kuwakatia tamaa, lakini kwa ushindi huo wana uhakika wa kubaki Ligi Kuu, kwani tayari umewapa wachezaji wao ari ya kupambana na kuleta matumaini mapya kwa mashabiki wao.

"Ushindi wa jana (juzi)umefufua matumaini ya mashabiki wetu, tuko kwenye Ligi Kuu takriban miaka 29, hatujawahi kushuka, matokeo tuliyokuwa tunayapata yalileta simanzi kubwa kwa mashabiki wa Mtibwa na wadau wa soka nchini, lakini ushindi wa jana (juzi), huku tukisaliwa na michezo minne, tunaweza kubaki kwa sababu matokeo haya yameongeza morali kubwa kwa wachezaji wetu na yameleta matumaini mapya kwa mashabiki wetu," alisema Kifaru.

Aliutaja ushindi huo kuwa haukuwa wa kubahatisha kwani wameifunga timu bora, iliyokuwa imesheheni wachezaji wakubwa kutoka mataifa mbalimbali ya nje ya nchi. "Tumeifunga timu yenye wachezaji wengi wakubwa kutoka mataifa mbalimbali ya nje, lakini pia tumecheza mpira mkubwa sana. Kuna watu walianza kutukatia tamaa wakisema tunashuka, mambo bado tutapambana kuhakikisha hatushuki," alisema Kifaru.

Pamoja na tambo za Kifaru na ushindi huo wa Mtibwa, lakini klabu hiyo inaendelea kuburuza mkia ikiwa imefikisha pointi 20 baada ya kucheza michezo 26 mpaka sasa.

Timu hiyo imebakisha michezo minne dhidi ya Yanga kesho kutwa, Mei 20 inatarajiwa kucheza dhidi ya Namungo siku tano baadae itaumana na Mashujaa FC na itamaliza msimu kwa kucheza na Ihefu kwenye uwanja wa Liti, Singida.

## Yanga yapania kutangaza ubingwa Dodoma

INATOKA UK. 24

ushindani mkubwa, ila sasa tumekaa vizuri kabisa, ukipiga mahesabu bado pointi nne hivi kuweza kuwa mabingwa, kwa hiyo niwaambie wanachama na mashabiki wetu kazi bado inaendelea, tuna mechi mbili dhidi ya Mtibwa Sugar na Dodoma Jiji, kama tukishinda hizi, basi ubingwa tutautangazia Dodoma," alisema Kamwe.

Endapo Yanga itashinda mechi yake ya Jumatatu dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro, itahitaji sare tu dhidi ya Dodoma Jiji ili kutawazwa kuwa wafalme wa nchi kwa mara ya tatu mfululizo.

Kama matokeo yatakuwa tofauti katika michezo hiyo miwili, basi Yanga itawabidi wasubiri mechi zingine mbili zinazofuata ili kuona uwezekano wa kutangazwa mabingwa kwa mara ya tatu mfululizo.

## Mgunda afichua siri mabadiliko Simba

INATOKA UK. 24

gea na wachezaji wake wote na kuwakumbusha umuhimu wa michezo iliyobakia na kuwataka kupambana kwa ajili ya timu bila kuangalia jambo lolote.

„Nashukuru wananisikiliza, nimekuwa nikiongea nao kama mzazi, huwa nawaambia kila mchezaji aliyesajiliwa na timu hii ana wajibu wa kucheza na kuitumikia, hii imesaidia hata wale ambao walikuwa hawapati nafasi ya kucheza, nikiwapa nafasi wananipa matokeo chanya," alisema Mgunda na kuongeza,

„Mfano mchezo wa jana (juzi) dhidi ya Azam, nilikaa na wachezaji na kuwakumbusha umuhimu wa mchezo huo, bahati nzuri na wenyewe walikuwa wanaitaka sana hii mechi, niliwaambia hii mechi ni muhimu sana kushinda kwa sababu itatupa kitu kuelekea kwenye michezo yetu ya mwisho, na wote tumeona kile wachezaji wangu walichokifanya.., kwa kweli nawapongeza sana," alisema Mgunda.

Alisema anajivunia wachezaji ambao walikuwa hawapati nafasi lakini kwa sasa kila anayempa nafasi anaenda kufanya kazi kubwa kwa ajili ya timu.

„Kwa sasa tunaangalia michezo inayofuata, tunashukuru kwa ushindi dhidi ya Azam, naamini tutaendelea kufanya vizuri kwenye michezo iliyobakia ili tuone mwisho wa ligi tutakuwa kwenye nafasi gani," alisema Mgunda.

Ushindi wa juzi umeifanya Simba kufikisha pointi 56 ikiwa ni pointi moja nyuma ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili nyuma ya vinara Yanga wenye pointi 68, hata hivyo Simba ipo nyuma kwa mchezo mmoja dhidi ya Azam na michezo miwili dhidi ya Yanga.

Michezo
Jumamosi Mei 11, 2024
Nipashe

Pickford asakwa Stamford Bridge UKURASA 22



# MGUNDA AFICHUA SIRI MABADILIKO SIMBA SC

●●●Aelezea namna alivyobadilisha upepo kwa wachezaji wake,sasa aahidi kuwa.....

**Na Faustine Feliciane**

KAIMU kocha mkuu wa klabu ya Simba, Juma Mgunda, amefichua kile ambacho amekifanya kwa wachezaji wake ambao sasa wamekuwa wakipambana uwanjani na kupata matokeo mazuri kwenye michezo yao ya Ligi kuu.

Mgunda amesema kuwaweka wachezaji wake karibu na kuongea nao kama mzazi kumesaidia kubadili upepo wa wachezaji wake na kupambana kumpatia matokeo mazuri kwenye michezo minne aliyoisimamia timu hiyo tangu kuondoka kwa kocha Mkuu Abdelhak Benchikha.

Katika michezo hiyo minne ambayo Mgunda amesimama kama kocha mkuu wa Simba, amepata ushindi kwenye michezo mitatu na kupata sare moja.

Mgunda alianza kwa sare ya bao 2-2 dhidi ya Namungo, akapata ushindi wa mabao 2-0 kwenye michezo dhidi ya Mtibwa Sugar na Tabora United kabla ya juzi kuifunga Azam FC mabao 3-0.

Mgunda alisema amekuwa akion-

INAENDELEA UK. 23



MGUNDA

# Yanga yapania kutangaza ubingwa Dodoma

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wamesema nia yao ni kutangaza ubingwa Mei 22, wakiwa Makao Makuu ya nchi, jijini Dodoma watakapocheza dhidi ya Dodoma Jiji kwenye uwanja wa Jamhuri.

Yanga imebakisha michezo minne ambapo katika hiyo itaanza kucheza na Mtibwa Sugar keshokutwa Manungu na baadae kwenda Dodoma kucheza na Dodoma jiji huku ikisaka pointi nne tu kuweza kutangaza ubingwa.

Ofisa habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema ingawa kwa sasa ligi imekuwa ngumu sana kwa kipindi hiki ambacho inaelekea ukingoni, watafanya kila njia kuhakikisha wanashinda mechi mbili zijazo ili watangaze ubingwa wakiwa Makao Makuu, Dodoma.

„Mechi za mwisho zina presha yake na ugumu wake,tunatarajia kupata

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >